# Nipashe

Jumanne Machi 23, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580528

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



JOHN MAGUFULI 1959 - 2021

JPM alitekeleza elimu nchini kwa staili kuziba ombwe kwa falsafa ya Nyerere

UKURASA 11

**Vilio** vyatawala bungeni

UKURASA 3



**Siri** ya namba 5 katika maisha ya Magufuli

UKURASA 3

# SAMIA: MIMI NDIYE RAIS

• **Aeleza** maneno ya mwisho ya JPM, Kenyatta asitisha hotuba..., marais wanena mazito... *Endelea ukurasa 2*









Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


Wakazi wa Jiji la Dodoma wakiuaga mwili wa Hayati Dk. John Magufuli, katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma jana. **Picha ndogo:** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, akimfariji mke wa aliyekuwa Rais Hayati Dk. John Magufuli, Mama Janeth Magufuli katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


**MICHEZO** **SIMBA ITAFIA KWA MKAPA - AS VITA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Samia: Mimi ndiye Rais

**Elizabeth Zaya na Agusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewaondoa shaka watu wanaodhani kuwa kwake mwanamke hawezi kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwahakikishia aliyesimama mbele yao ni rais mwenye maumbile ya mwanamke.

Aliwahakikishia maelfu ya wananchi na viongozi wa kitaifa, kimataifa waliohudhuria mazishi ya kitaifa ya Hayati Dk. John Magufuli, katika viwanja vya Jamhuri, jijini Dodoma.

"Wale ambao wana mashaka mwanamke huyu ataweza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nataka niwaambie aliyesimama hapa ni Rais..."

"Nataka nirudie kwamba aliyesimama hapa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye maumbile yake ni mwanamke," alisisitiza Rais Samia.

Kauli ya Rais Samia imekuja baada ya marais kutoka nchi mbalimbali za Afrika na viongozi waliowakilisha marais wao kutoa salamu zao za rambirambi na kumwahidi kumpa ushirikiano katika kipindi chote atakachokuwa madarakani.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba Kabudi, aliyekuwa mshereheshaji wa shughuli hiyo, alimwomba Rais Samia kuzungumza na wananchi baada ya viongozi hao wa kimataifa kuzungumza kabla ya kupata fursa ya kuuaga kwa mara ya mwisho mwili wa Hayati Rais Dk. John Magufuli.

Rais Samia akizungumzia mazungumzo yake ya mwisho na Hayati Magufuli, wakati akiwa kwenye ziara mkoani Tanga, alisema; "Nilipata fursa ya kuongea na Dk. Magufuli siku chache kabla ya kifo chake pale nilipomtaarifu kwamba naenda Tanga kwenye ziara, aliniambia, Samia usiwe na wasiwasi, naendelea vizuri, nenda kafuatilie utekelezaji wa Ilani ya CCM kama tulivyoahidi tutaitekeleza. Wape salamu zangu waambie nawapenda."

Rais Samia alisema, hakuamini kama siku ile ndiyo ingekuwa ya mwisho kuzungumza naye.

"Hayo ndiyo yalikuwa maneno yake na mimi ya mwisho, sikujua kama maneno yale yalikuwa ya kuniaga na kuwaaga Watanzania," alisema Rais Samia.



"Sikujua kwamba sitapokea simu yake tena, zile simu za asubuhi za kusema wewe amka nenda kafanye hili na lile. Sikujua kama simu hazitakuja tena, sikujua kama sitosoma mwandiko wake tena."

"Sikujua kama sitoonana naye tena kushauriana naye tena. Ni jambo ambalo litanichukua muda mrefu kulizoea," alisema huku akimshukuru kwa upendo na imani yake.

"Namshukuru kwa upendo na malezi yake kwangu. Kwa pamoja vimeniandaa kupokea kijiti cha uongozi kutoka kwake, ametupika, tukawiva," alisema Rais Samia.

"Nimehuzunishwa sana na kifo cha Rais Magufuli, nenda baba. Umevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo umeumaliza.

**ALIMWANDAA KIMATAIFA**

Akimzungumzia Dk. Magufuli, alisema alimwandaa katika uongozi wa kimataifa na kwamba hana shaka na eneo hilo.

"Dk. Magufuli aliniandaa sana katika eneo la uhusiano wa kimataifa, mara nyingi alikuwa akinitumia, ni kama alijua, akaniandaa, na hawa wote mnaowaona hapa ni kaka zangu ni marafiki zangu wa karibu sana," alibainisha Rais Samia.

**KENYATTA ATII ADHANA**

Katika tukio lingine, Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, wakati akitoa salamu za Wakenya, alilazimika kunyamaza kwa dakika mbili na sekunde 30 ili kupisha adhana ya swala ya adhuhuri kutoka Msikiti wa Gadafi.

Huku watu waliokuwa wakifuatilia salamu hizo kwenye televisheni zao wasielewe kilichotokea kwa Rais Kenyatta kunyamaza ghafla. Ilipopita adhana hiyo, Rais Uhuru aliomba radhi kwa wananchi kwa kitendo cha kusitisha ghafla hotuba yake na kuendelea kutoa salamu zake kitendo kilichoangaliwa na umati wa watu waliojitokeza katika uwanja huo.

**NYUSI AMUENZI JPM KWA KUZUNGUMZA KISWAHILI**

Katika hatua nyingine, Rais wa Msumbiji, Filipe Nyusi, aliwashangaza wananchi waliojitokeza katika mazishi hayo kwa kutoa salamu za rambirambi kwa lugha ya Kiswahili fasaha kuanzia mwanzo hadi mwisho wa salamu zake.

Kwa muda wa dakika tatu alizozitumia kutoa salamu, alizungumza Kiswahili hali iliyowashangaza wananchi wengi kutokana na nchi yake kutumia lugha ya Kireno kama lugha ya mawasiliano, ikiwa ni namna ya kumuenzi hayati Magufuli, aliyehakikisha lugha hiyo inatumika SADC kama lugha rasmi.

# Marais wanena mazito

**Agusta Njoji na Elizabeth Zaya**

MARAIS wa nchi mbalimbali wameeleza namna Hayati John Magufuli alivyokuwa shujaa kwenye uongozi wake na alivyokuwa akihamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili Afrika.

Viongozi hao walitoa salamu hizo jana wakati wa shughuli ya mazishi kitaifa iliyofanyika katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, na kuhudhuriwa na marasi tisa na viongozi wengine zaidi ya 50 waliowakilisha nchi zao.

**RAIS KENYA**

Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, alisema Hayati Magufuli, alikuwa rafiki yake wa karibu na walikuwa wakiwasiliana mara kwa mara mchana jioni wakibadilishana mawazo kuhusu nchi zao.

Kenyatta ambaye ni Mwenyekiti wa Afrika Mashariki (EAC) akizungumza kwenye mazishi ya kitaifa ya Hayati Magufuli, alisema kifo hicho kwake yeye ni pigo.

"Sisi kama Wakenya na mimi binafsi nilisema liwe liwalo lazima niungane nanyi kumsindikiza ndugu yetu na niwahakikishie tutaendelea kufanya kazi pamoja kuleta Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki na Bara la Afrika pamoja," alisema.

"Rais mwenzangu, Samia Suluhu Hassan barabara umeonyeshwa na imefunguliwa, niseme kwa dada angu Samia na sasa ni Rais mwenzangu, umeonyeshwa barabara mwito unao Hapa ni kazi tu, wananchi wa Tanzania wapo nyuma yako tunachoomba mwendelee na umoja na mmuunge mkono Rais wenu endeleze kazi iliyobaki na tujivunie kazi iliyoanzishwa na mwenzetu."

Rais Kenyatta alisema, Rais Magufuli ameheshimika si Tanzania pekee bali pia Afrika Mashariki na duniani.

Alisitisha hotuba yake kwa dakika kadhaa kupisha adhana.

"Kwa muda wa miaka michache ameonyesha sisi kama wa Afrika tupo na uwezo wa kujitoa katika kutegemea watu wa nje na tupo na uwezo kama Waafrika kusimamia uchumi wetu na kuhakikisha wananchi wetu wametendewa haki, kwa muda mfupi tumeona kazi ya ujenzi wa barabara na mambo mengine mengi ambayo itasaidia Watanzania na sisi wa Afrika Mashariki," alisema.

**RAIS AFRIKA KUSINI**

Rais wa Afrika ya Kusini, Cyril Ramaphosa, alitaja mambo matatu ambayo anamshukuru Magufuli, ikiwamo kuwa shujaa dhidi ya rushwa na ubadhirifu na kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Mengine ni shabaha yake ya kukomboa nchi yake kiuchumi pamoja, kikanda na barani Afrika. Alisema ameondoka kiongozi mahiri ambaye alikuwa analenga kulikomboa Bara la Afrika na ni shujaa wa Afrika.

Alisema ni kiongozi mahiri katika kizazi kipya ambaye amesimama kupambana na rushwa na kwamba viongozi hawapaswi kujitumikia bali kutumikia mataifa yao.

**RAIS WA MALAWI**

Rais wa Malawi, Lazarus Chakwera, alisema ni vema jina la Dk. Magufuli likahifadhiwa katika makabati ya Afrika na katika vijiji vya nchi hizo ili kuendelea kukumbuka na kutoka kwake kama kiongozi bora katika kusimamia nidhamu.

"Tuliopata dhamana ya kuendesha mataifa yetu, uongozi wa Dk. Magufuli ni mfano na tutaendelea kuutumia ili uendelee kutufundisha na kutuondolea uzembe, alikuwa si tu nyota bali alikuwa ni shujaaa, jina lake linatakiwa kuhifadhiwa katika makabati yote ya Afrika kama alama ya Afrika tunayoihitaji na matendo yake yafutwe katika kila kijiji cha Afrika," alisema Chakwera.

**RAIS WA ZAMBIA**

Rais wa Zambia, Edgar Lungu, alisema Dk. Magufuli atakumbukwa kwa uhusiano waliouimarisha kati ya nchi hizo mbili.

Alimtaja kama mtu aliyekuwa amenyooka katika maamuzi yake na kwamba alikuwa mwanamageuzi asiye na hofu.

**RAIS WA ZIMBABWE**

Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, alisema Zimbabwe wamepoteza rafiki wa nchi yao na kaka na kwamba alikuwa Mwafrika aliyeamini kwamba Afrika ni lazima ifanye biashara na kujiendeleza kiuchumi.

Alisema Dk. Magufuli ameharakisha maendeleo ya kiuchumi nchini mwake na kwamba katika kipindi akiwa Mwenyekiti SADC aliweka msisitizo katika maendeleo ya viwanda na kutengeneza ajira.

Alisema watu wa Zimbabwe watamkumbuka kwa kuamua kutenga tarehe 25 kama siku ya kuinua sauti dhidi ya vikwazo ambavyo nchi hiyo iliwekewa.

**RAIS COMORO**

Kwa upande wake, Rais wa Comoro, Azali Assoumani, alisema alikuwa ni kiongozi ambaye siku zote hakusita kusikiliza matatizo ya nchi hiyo.

"Mamlaka aliyoyapata dada angu Rais Samia ataweza kutimiza mahitaji ya Watanzania, ninatamani na atakuwa ni mrithi wa kweli wa Rais Magufuli kwa kuimarisha amani na kuleta maendeleo kwa kanda yetu ya Afrika," alisema.

**MAKAMU WA RAIS BURUNDI**

Makamu wa Rais wa Burundi, Prosper Bazombaza, alisema alikuwa kiongozi wa Waafrika kwa ujumla na amepotea mtu mwenye maono na msimamo.

Alisema alijikita kupambana na rushwa na kumwomba Rais Samia kuhakikisha anaendeleza yaliyoanzishwa na Hayati Magufuli na kuanzisha miradi mipya ili Tanzania isirudi nyuma.

**WAZIRI MKUU RWANDA**

Waziri Mkuu wa Rwanda, Edouard Nigirente, alisema serikali yake ilifanya kazi kwa karibu na Hayati Magufuli na alijitoa kuimarisha uhusiano kati ya nchi hizo mbili na historia yake itakumbukwa daima.

**RAIS WA MSUMBIJI**

Rais wa Msumbiji, Filipe Nyusi, alisema Dk. Magufuli alitumia wadhifa wake kwa uhodari katika kuiongoza SADC na kwamba kuondoka kwake gafla kumeacha pengo kubwa.

"Kuishi kwake katika upendo katika jamii yake na utoaji maoni yake ni alama ambazo haziwezi kufutika kamwe, heshima milele tutazitunza," alisema.

"Nakumbuka Dk. Magufuli alikuwa anapiga simu saa kumbi na mbili asubuhi akiniambia amka ndugu yangu hapa kazi tu, nakumbuka tulipokutana hivi karibuni Chato tulijadiliana namna ya kuendeleza usalama na utulivu kwenye Kanda ya Tanzania na Msumbiji."

Alisema wanaamini kwamba Rais wa sasa wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan ataendeleza ushirikiano uliokuwapo, kuwaunganisha Watanzania, Waafrika na kuendeleza yale yaliyoachwa na Dk. Magufuli.

**RAIS WA BOTSWANA**

Rais wa Botswana, Mokgeetsi Masisi, alisema wamepoteza kiongozi wa kweli na mahiri aliyeiongoza nchi yake na Afrika katika masuala ya uongozi wa demokrasia.

"Tutamkumbuka kwa michango yake na juhudi zilizokuwapo katika kuleta amani katika Jamhuri ya Kidemokrasia na Congo (DRC)," alisema Rais Masisi.

"Mama Samia una viatu vikubwa vya kuvaa lakini hapana shaka ukiwa kama mwanamke pekee, daima tutakuunga mkono katika manufaa na mafanikio ya Tanzania kwa sababu mafanikio ya Tanzania ndiyo yetu pia."

# Simanzi bungeni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SIMANZI, majonzi na vilio jana vilitawala katika viwanja vya Bunge wakati wa tukio la kuaga na kutoa heshima za mwisho kwa hayati Rais John Magufuli, huku Spika wa Bunge Job Ndugai, akifichua siri alivyopigiwa simu na Magufuli akitaka azikwe wapi.

Spika Ndugai, alisema kutokana na kifo hicho nchi imegubikwa na huzuni kubwa kwa kuwa Watanzania wamempoteza kiongozi wao mahiri na mtu wa watu.

"Jukumu letu kama taifa ni kuendelea kumwombea mpendwa wetu, leo hii ningependa kuwapa nafasi hata wabunge watatu kutoa salamu zao, lakini muda hautoshi hivyo basi tarehe 30, wakati wa Bunge tutaweka utaratibu na tutakuwa na azimio letu sisi kama Bunge juu ya tukio hilo," alisema Ndugai.

Ndugai alisema hayati Rais John Magufuli amekuwa sehemu ya Bunge kwa miaka 26 na kwamba tukio la kuuaga mwili wake limekuwa ni majonzi makubwa kwa Bunge.

"Lango hili la Bunge au lile la ukumbi wa Msekwa ndilo amekuwa akilitumia Hayati Rais Magufuli, kwa kipindi chote cha miaka 26, toka akiwa mbunge kuanzia mwaka 1995 leo hii ni siku ya majonzi makubwa sana kwetu sisi wabunge, kwani tumehelemewa, tumechanganyikiwa Watanzania wanalia na sisi tunasema asante Mungu kwa kutupa Magufuli," alisema Ndugai.

### HALI ILIVYOKUWA

Mwili uliwasili katika viwanja vya Bunge majira ya saa 2:05 asubuhi na baada ya baadhi ya wabunge kuuona msafara wa magari yaliyokuwa yakiusindikiza mwili huo walianza kuangua vilio kwa sauti za juu.

Mwili uliposhushwa katika viwanja vya Bunge, Spika wa Bunge Job Ndugai, aliwaomba wabunge watulie ili ratiba ya kuaga na kutoa heshima za mwisho ianze. Wabunge watatu walipewa nafasi na kufanya ibada fupi ya kuuombea mwili wa hayati Rais John Magufuli.

Wa kwanza alikuwa Shally Raymond, ambaye ni Mwenyekiti wa Wabunge Wakatoliki, aliendesha ibada fupi na kuwataka wabunge kuendelea kumwombea Hayati Rais Magufuli na kumsamehe kwa yale aliyowakwaza wakati wa uhai wake.

Anna Lupembe, alipewa nafasi ya pili akiwa ni Mwenyekiti wa Jumuiya Waprostanti bungeni ambaye alitoa pole kwa mama Janeth Magufuli na Watanzania kwa ujumla na kumwomba Mungu ampatie pumziko la milele.

Pia Mbunge wa Wete, Omari Ally Omari, alipewa nafasi ya kusoma dua kwa niaba ya wabunge Waislamu na kuwataka wabunge kuungana na kumwombea Hayati Rais Magufuli, ili Mungu aipumuzishe roho yake kwa amani.

Baada ya wabunge hao, Spika Ndugai alimpa nafasi Naibu Spika Dk. Tulia Ackson, ambaye alisema uwapo wake katika kiti hicho, umechangiwa na Hayati Rais Magufuli kwa kiasi kikubwa.

"Vitabu vya dini vinasema kuwa upumbavu wa Mungu ni hekima ya mwanadamu, yale mema ambayo wengine hawajayaona sisi tumeyaona," alisema.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alisema kuwa hawezi kuongea wakati akiendelea kuona mwili wa hayati Rais Magufuli ukiwa mbele yake kwenye jeneza.

"Wabunge naomba mnisamehe sana siwezi kuongea wakati naendelea kumuona kiongozi wangu aliyekuwa akinipigia simu kila mara kunipa maagizo leo hii amelala hapa mbele yetu," alisema Majaliwa kwa masikitiko.

# Siri namba 5 maisha ya JPM

**Na Salome Kitomari**

HAYATI Rais Dk. John Magufuli, ameacha siri kubwa ya alama ya namba tano katika safari yake ya miaka 61 aliyoishi duniani.

Siri ya namba tano katika safari ya uongozi ya maisha ya Hayati Rais Dk. John Magufuli, ilianzia wakati aliposhika madaraka ya kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Awamu ya Tano, alipoapishwa Novemba 5, 2015.

Namba 5 ilichomoza tena mwaka 2020 aliposhinda muhula wa pili na kuapishwa Novemba 5,2020.

Katika safari yake ya mwisho kwenye Jiji la Dar es Salaam, mwili wake ulizungushwa mara tano katika uwanja wa Uhuru na Dodoma pia ulizungushwa mara tano katika uwanja wa Jamhuri.

Katika tukio la kihistoria la kusherehekea maisha yake duniani, juzi mwili wake ulizungushwa mara tano katika Uwanja wa Uhuru, Jiji la Dar es Salaam ikiwa ni kumuenzi na kutoa fursa kwa Watanzania kumuaga kwa pamoja baada ya wengi kushindwa kupita mbele ya jeneza kutokana na msongamano.

Namba tano ilijitokeza tena siku ya mazishi yake kitaifa katika viwanja vya Jamhuri jijini Dodoma, baada ya kukamilika kwa ibada takatifu na salamu za wakuu wa nchi mbalimbali duniani, mwili wake kuzungushwa mara tano katika uwanja huo ili watanzania wamuage.

Pia, mwili wa kiongozi huyo ulitembezwa katika mitaa mitano ya Jiji la Dodoma, kutoa nafasi kwa wakazi wake kuuaga.

Jana Msemaji wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, alitangaza utaratibu mpya ambao gari lililobeba mwili wa Hayati Dk. Magufuli kupitishwa sehemu waliyokaa wananchi nao kuaga kwa kupunga mkono na kumuenzi mpendwa wao.

### Na. 5 KIBIBILIA INAMAANA GANI?

Kwa mujibu wa Blog ya Injili Tanzania, taarifa ya fahamu namba kibiblia na maana zake katika ulimwengi wa roho na mwilini, namba tano ina maanisha wokovu au hukumu. "Yesu alipata hukumu ili tupate Wokovu kwa hiyo usishagae namba tano ikiwakilisha wokovu au hukumu kwa wakati mmoja. Namba tano inaonekana robo. Namba ya kumi, tano inaweza kuwa kama tano, 50, 500, 5,000," imeandikwa.


*Umoja wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afisa wa Kupambana na Fedha Haramu*

*Msese Road Plot 96, Kinondoni*
*Tel.No.:+255-22 - 266 7895*
*Tel:No.:+255-22 - 266 7679*
*Fax.No.:+255-22 - 266 8745*
*Email: executivesec@esaamlg.org*
*Web: www.esaamlg.org*

*Office of the Executive Secretary*
*ESAAMLG*
*P.O. Box 9923 Dar es Salaam,*
*TANZANIA*

# RAMBIRAMBI



**Mh. Dkt John Pombe Joseph Magufuli**
**1959 – 2021**

Baraza la Mawaziri, Kikosi Kazi cha Maofisa Waandamizi na Wafanyakazi wa Umoja wa Nchi za Mashariki na Kusini Mwa Afrika wa Kupambana na Fedha Haramu wamepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt John Pombe Joseph Magufuli.

Tunatoa Salaam za pole kwa Rais Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan na Serikali yote, Mama Janet Magufuli na Familia yake na Watanzania wote kwa ujumla.

***Roho ya Marehemu ipate Rehema kwa Mungu na ipumzike kwa Amani.***

**Eastern and Southern Africa**
**Anti – Money Laundering Group**
**ESAAMLG Secretariat**
**Website: www.esaamlg.org**



**UNHCR**
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**INVITATION TO BID: NO. RFP/2021/SUP/012 FOR THE ESTABLISHMENT OF FRAME AGREEMENTS FOR PROVISION OF ROAD CARGO AND PASSENGER TRANSPORT SERVICE FROM KIGOMA REGION TO BURUNDI**

**1. Background:**

The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Dar es Salaam invites reputable and qualified suppliers to submit firm offers for establishment of a frame agreement for the provision of road cargo and passenger transport service from Kigoma region to Burundi

**2. Eligibility:**

Suppliers duly registered with relevant government authorities, with sound financial basis, relevant experience, reputed clientele and with knowledge of how to meet UNHCR's requirements are invited to participate in the bidding process.

Kindly download the tender documents in the below link:

**https://drive.google.com/drive/folders/1VaGAGyMV9NQ1xP1XPGIJktVIOc9tZr0R?usp=sharing**

If you fail to access the link, please write to ishobeza@unhcr.org copy ndassa@unhcr.org

**CRUCIAL DATES FOR THIS REQUEST FOR PROPOSAL**

| | |
|---|---|
| Pre-bid Conference meeting will be held | Monday 30th March 2021 |
| Deadline for receiving requests for clarification | Friday 11th April 2021 at 2359hrs EAT |
| Deadline for submission of offers | Wednesday 27th April 2021 at 1600hrs, EAT |

*UNHCR tenders are free of charge, no fees are charged to collect the tenders.*

# Vyumba vya madarasa kulaza wageni Chato

**Na Richard Makore,** CHATO

VYUMBA vya madarasa vinatarajiwa kutumika kulaza wageni watakaofika wilayani Chato mkoani Geita kwa ajili ya kushiriki shughuli ya maziko ya aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hyati Dk. John Magufuli yanayotarajiwa kufanyika Ijumaa nyumbani kwake.

Akizungumzia utaratibu huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato, Eliud Mwakiteleko, alisema wanafanya vikao ili kuangalia suala hilo. Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana mjini Chato, Mwakiteleko alijibu kwa kifupi kwamba bado wanajadili suala hilo.

Jana shule mbalimbali zilifungwa Ili kuombelezo kifo cha Dk. Magufuli ambaye aliagwa kitaifa jijini Dodoma.

Kwa upande wake, mfanyabisahara mjini Chato, Pascally Lutandura alisema amenunua magodoro madogo ambayo yatawekwa kwenye madarasa ili kulaza wageni.

Alisema ameamua kufanya hivyo ili kuhakikisha wageni watakaofika Chato wanapata sehemu ya kulala mpaka siku ya kuzika. Aliongeza kuwa utaratibu huo utasaidia baadhi ya wageni ili waweze kupata sehemu za kufikia na kulala kuwawezesha kushiriki maziko.

Wakati huo huo, umoja wa waendesha bodoboda wilayani Chato umeandika barua kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, kuomba kibali cha kushiriki katika maziko hayo.

Mwenyekiti wa umoja huo, James Andrew akizungumza na Nipashe alisema, hayati Magufuli wakati wa uhai wake aliwasaidia vijana wengi.

Alisema alihakikisha kazi hiyo inakuwa ya heshima pamoja na kuwakopesha Sh. milioni 10 ambazo walizitumia kununua bodaboda nne ambazo kwa sasa zinawaingizia kipato.

Andrew alisema wakipewa kibali wanatarajia jumla ya bodaboda 600 zilizopo wilayani Chato zitashiriki ili kumuenzi hayati Magufuli.

Aliomba vyombo vya ulinzi na usalama kuwawekea utaratibu ambao utawawezesha kushiriki bila kuingilia mambo mengine.



Mkurugenzi Mtendaji wa IRUWASA, Mhandisi David Pallangyo, akiongea na waandishi wa habari jana ofisini kwake ikiwa ni wiki ya maji. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

## Walala nje ya uwanja kusubiri kuaga mwili

**Peter Mkwavila na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKAZI kutoka vijiji vya wilaya za Mkoa wa Dodoma na mikoa jirani, waliamua kulala karibu na Uwanja wa Jamhuri ili kuwahi kuuaga mwili wa Hayati Rais John Magufuli.

Wakizungumza na Nipashe uwanjani hapo kwa nyakati tofauti, walisema wamelazimika kulala kwenye maeneo hayo kutokana na wengi wao kutembea kwa miguu umbali mrefu kutoka vijijini baada ya kukosa usafiri wa uhakika wa kuwafikisha kwa haraka.

"Asilimia kubwa unao waona hapa tumelazimika kulala nje ya uwanja na wengine wameomba kwa walinzi binafsi wanaolinda vibanda vya kuuzia mbao na ofisi za watu zilizopo eneo la uwanja huu, tumetoka vijiji mbalimbali na tumetembea zaidi ya kilometa 50, ili tu tuweze kuwahi na kumuaga rais wetu ambaye ni mkombozi wa wanyonge," alisema Matonya Odoba.

Barabara zinazozunguka uwanja hao ikiwamo ya Singida, Morogoro, Iringa na Arusha, zilifurika kwa idadi ya watu.

Walinzi wa usalama walijikuta wakipata wakati mgumu kutokana na msongamano wa kuwapanga watu ambao wakati mwingine walilazimika kuzuia vyombo vya usafiri kupita.

Madereva wa daladala zinazotoka maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma, walilazimika kushusha abiria wao nje ya mji na kutembea kwa miguu hadi uwanjani.

Baadhi ya nyimbo zilizokuwa zikiimbwa na waombolezaji ni zenye ujumbe "Tunakulilia mwamba uliyefanya mambo makubwa tangulia, Mungu akupe pumziko la milele, tutaendelea kukukumbuka na utabaki mioyoni mwetu."

# Utata wagubika waliokufa kuaga mwili wa JPM Dar

**Christina Mwakangale na Maulid Mmbaga**

UTATA umegubika juu ya idadi ya watu waliofariki katika Uwanja wa Uhuru wakati wa shughuli za kuaga mwili wa za aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli jijini Dar es Salaam juzi.

Hata hivyo, Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), imetoa taarifa ya watu saba kujeruhiwa ikiwamo kifo cha mtu kimoja hospitalini hapo, kwa kile kilichoelezwa ni kukanyagana kutokana na msongamano wa maelfu ya wananchi waliojitokeza kuaga mwili. Baadhi ya ndugu waliopoteza ndugu zao walizungumza na Nipashe na kueleza kuwa watu saba wamefariki, wakiwamo watano wa familia moja kati yake watoto wanne.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma MNH, Aminiel Aligaesha, alithibitisha kupokea majeruhi hao na kulazwa jana, akiwamo mtoto wa miaka 13 pamoja na mwili wa mwanamke mwenye umri wa miaka 53.

Tukio hilo lilitokea juzi kwenye Uwanja wa Uhuru, jijini Dar es Salaam, ambao ulikuwa ni maalum kwa shughuli za kuaga mwili na kuruhusu wakazi wa jiji kwa siku mbili, Machi 21 na 22, mwaka huu, kumuaga Hayati Rais Magufuli.

Aidha, taarifa za awali zilizoifikia Nipashe, zilisema watu wengi walipoteza maisha katika tukio hilo, juzi.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa alipotafutwa na Nipashe, alisema taarifa zaidi zitatolewa leo.

### NDUGU WAZUNGUMZA

Akizungumza na Nipashe mmoja wa mwanafamilia aliyopotelewa na ndugu, Denis Mtuwa alisema walipotelewa na wapendwa wao watano, ambao wote walihudhuria na kuuaga mwili wa Hayati Magufuli.

Alisema wapo katika jitihada za kufuatilia miili hiyo katika hospitali walipohifadhiwa ndugu zao ili taratibu za mazishi ziendelee.

"Tatizo lililojitokeza limetushtua sana, kwani hatukutegemea kuwapoteza ndugu zetu kwa idadi hiyo ndani ya familia moja na taratibu za mazishi zinaendelea sambamba na kuichukua miili kutoka kule ilipohifadhiwa Temeke," alisema Mtuwa.

Sadiki Hussein, mkazi wa Chanika ambaye alimpoteza ndugu yake aliyetambulika kwa jina la Mariam Hussein (22), alisema, marehemu aliacha mtoto mmoja mwenye umri wa miaka mitatu.

"Tumesha upata mwili wa ndugu yetu na tumeuhifadhi katika Hospitali ya Temeke na taratibu za mazishi zinaendelea na tunategemea kusafirisha leo, kwenda Morogoro kwa ajili ya mazishi."

### KANDA MAALUM

Mbali na kauli ya Kamanda kuwa atatoa ufafanuzi leo, chombo kimoja cha habari kilimnukuu Mambosasa akisema, baadhi ya wananchi walioshiriki shughuli ya mazishi katika kumuaga hayati Magufuli walijeruhiwa baada ya kukanyagana.


Alisema idadi ya watu waliojeruhiwa katika shughuli hiyo ni wengi, ingawa hakuwa na takwimu halisi siku ya jana.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma MNH, Aligaesha, alifafanua waliopokelewa hospitalini hapo jana, kutokana na tukio hilo, juzi.

Alisema majeruhi waliofikishwa ni Aza Hamisi (26), Josseh Sunne (30), Andrew Mirambo (26), Hawa Adam, Beatrice Mdake (44), mtoto wa miaka 13 ambaye yeye pamoja na mwanaume mmoja hawakufahamika majina yao.

Pia alisema kati ya majeruhi hao wanne wamehamishiwa Taasisi ya Tiba ya Mifupa, Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI) kwa uchunguzi, huku mwili wa marehemu Rose Shabakaki mwenye umri wa miaka 53, ukihifadhiwa.

TANGAZO


NMB
Karibu yako
Pumzika kwa Amani
Tutakukumbuka daima kwa maono yako na msimamo madhubuti wa kujenga na kulinda nchi yetu.
Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli
1959 - 2021
www.nmbbank.co.tz

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Kwenye misongamano watoto wasiruhusiwe

**ZIPO** taarifa za watu kadhaa kupoteza maisha katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, kutokana na kukanyagana na msongamano.

Ipo familia hadi sasa imethibitisha kupoteza watoto watano, mama na dada wa kazi ambao wote walikuwa uwanjani kwa ajili ya kuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli, lakini kutokana na msongamano.

Bado Jeshi la Polisi halijatoa taarifa rasmi, lakini tayari familia zimethibitisha kupoteza wapendwa wao na baadhi kujeruhiwa kwenye tukio hilo.

Hili ni tukio la kusikitisha sana kwa kuwa linakumbusha majonzi ya tukio la watu kupoteza maisha kwenye msongamano ambao walikwenda kukanyagana kwa lengo la kupata mafuta ya upako mjini Moshi. Kati ya waliofariki baadhi walikuwa watoto.

Inafikirisha sana kwamba inakuwaje mzazi anabeba watoto wengi na kwenda nao kwenye msongamano mkubwa kama huo, ambao kwa hali ya joto la Dar es Salaam ni rahisi kukosa hewa au mvua ikinyesha ni ngumu kulinda usalama wa watoto.

Juzi kupitia vyombo vya habari tuliona idadi kubwa ya watu uwanjani humo kiasi cha wengine kushindwa kuaga kutokana na kukosekana muda kutotosha, huku wengine wakisukumana kiasi cha kukosa pa kusogeza mguu.

Kunapokuwa na hatari kila mmoja hujitahidi kuokoa nafsi yake na kwa watoto ni ngumu kujitetea dhidi ya nguvu ya watu wazima na kusukumana kulikokuwapo. Hivyo haikuwa salama kabisa kupeleka watoto kwenye tukio kama lile.

Tunaona siyo sawa na ni hatari sana kwa watoto kupelekwa kwenye matukio ambayo siyo lazima na wangeweza kutazama wakiwa nyumbani kupitia runinga au mitandao ya kijamii.

Kupeleka watoto kwenye mikusanyiko hiyo ni hatari sana kwa kuwa ni rahisi kwa udogo wao kukosa hewa na kupoteza maisha kama ilivyojitokeza kwa watoto hao.

Kwa kuwa shughuli ya kuaga mwili wa kiongozi huyo inaendelea hadi Ijumaa (Machi 26, mwaka huu), ni muhimu msisitizo ukawa ni watu wazima pekee kwenda viwanjani na watoto kusalia nyumbani, ili kuona tukio hilo kupitia runinga na mitandao ya kijamii.

Haipendezi na ni hatari sana kupeleka watoto kwenye matukio haya, ambayo huleta idadi kubwa ya watu kwa wakati mmoja kwa kuwa lolote linaweza kujitokeza na kusababisha maafa kama ambavyo ilijitokeza juzi.


Ni muhimu sana kuchukua tahadhari na kujifunza kuhusu matukio haya ambayo kwa kiasi kikubwa hugharimu maisha ya watu, lakini ni muhimu serikali kuweka utaratibu maalum ikiwamo kuzuia watoto kwenda kwenye matukio haya, na badala yake kuangalia kupitia vyombo vya habari.

Kutokana na ukuaji teknolojia, taarifa zinarushwa kila mahali kama kwenye runinga na mtandaoni. Hili ni tukio la kitaifa linaonyesha na taarifa zinapatikana, hivyo hakuna sababu ya kukusanya watoto na kuwapeleka uwanjani.

Tukio hili limeacha funzo ni muhimu kujifunza na kuchukua hatua kuhakikisha usalama wa watu wote kunapokuwa na msongamano.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

## Kuchapa wanafunzi viboko sawa, ila vigezo na masharti ni muhimu

**SUALA** la ama kuwapo au kutokuwapo adhabu ya viboko shuleni, ni mjadala mpana katika jamii, ambao umegawa watu katika makundi mawili, wakiwapo wanaounga mkono adhabu hiyo na wengine wanaipinga.

Adhabu hiyo imekuwa ni mjadala mpana, kutokana na matukio ya kuumizwa kwa baadhi ya wanafunzi, hivyo kuwafanya wadau wa elimu kutoona umuhimu wake na wengine kuamini kwamba, bado adhabu hiyo inafaa.

Hadi sasa, kuna sheria mahsusi inayosimamia viboko nikiwa na tafsiri halisi.

Katika msimamo wake, Rais Dk. John Magufuli, enzi ya uhai wake, ziarani mkoa wa Mbeya wakati huo, alitamka nafasi ya viboko, pale Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alipowachapa wanafunzi 392 wa shule moja ya sekondari kwa tuhuma za kuchoma moto mabweni ya shule hiyo.

Mbali ya kupewa adhabu, wanafunzi hao walitakiwa kulipa Sh. 200,000 kila mmoja kwa ajili ya kukarabati mabweni mawili, ambayo walituhumiwa kuyateketeza kwa moto.

Binafsi ninaungana na kauli hiyo, kwa kuwa adhabu ya viboko kwa mwanafunzi, si mbaya kama itatolewa kwa lengo la kumrekebisha, lakini ikiwa ya kumkomoa mwanafunzi, matokeo yake ni kuumia na kusababisha mjadala uliopo sasa.

Suala la kuwapo adhabu ya viboko kwa wanafunzi ni jambo la kawaida, pale inapotolewa kwa utaratibu sahihi na inawezekana kupunguza matukio ya uharibifu wa mali za shule na mengine mengi yasiyotakiwa.

Vilevile, adhabu hiyo ikitolewa kwa utaratibu unaotakiwa, itapunguza pia matukio mbalimbali ya athari ya viboko kwa wanafunzi shuleni kama vile kuumizwa kwa baadhi yao na hata kuachwa na makovu.

Ni jukumu la mzazi na mlezi kumpa fursa ya kusoma mtoto wake, pia mwalimu anatakiwa kutimiza wajibu wake kwa uadilifu wa kumpa elimu, kumtunza, kumlea na kumwongoza kwa kumkuza na kumwendeleza.

Si dhamira ya mwalimu kumdhuru mwanafunzi kwa kumuadhibu, bali kumjenga na kumrekebisha, kwa kuwa mwalimu ni mlezi wake awapo shuleni, hivyo hata adhabu anayotoa inatakiwa kumrekebisha na siyo kumkomoa.

Hata Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Ufundi, Prof. Joyce Ndalichako, alishaonyesha kukerwa na baadhi ya walimu wanaoshindwa kufuata mwongozo wa adhabu ya viboko shuleni.

Mwongozo huo upo katika waraka wa kiserikali, unaoweka wazi kuwa adhabu ya viboko na inaweza kutolewa, endapo kutatokea utovu wa nidhamu uliokithiri ama makosa ya jinai yaliyotendeka ndani au nje ya shule na yenye mwelekeo wa kuishushia shule heshima.

Pia inaelekeza kwamba adhabu ya viboko itakayotolewa sharti izingatie ukubwa wa kosa, umri, jinsi na afya ya mtoto na isizidi viboko vinne kwa wakati mmoja.

Anabainisha kuwa, waraka unaomtambua mwalimu mkuu au mkuu wa shule, ndiye mwenye mamlaka ya kutoa adhabu ya viboko, pia atie saini katika kitabu maalum kila adhabu ya viboko inapotolewa.

Waziri anasema, waraka huo unaweka wazi kuwa, mwanafunzi ama mzazi anapokataa adhabu ya viboko, sharti asimamishwe shule ili kupisha hatua nyingine za kinidhamu juu ya kosa lake.

Walimu wanaonywa kuwa hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yao, kama watakiuka utaratibu ulioidhinishwa na waraka huo, na ni marufuku kuonekana wakiwa na fimbo mkononi kwa lengo la kumwadhibu mwanafunzi.

Muungwana anaamini kwamba, kutozingatia mwongozo huo, ndiyo chanzo cha kuwagawa watu na kuzusha mjadala katika jamii wa kutaka adhabu ya viboko iendelee ama ifutwe.

Wakati uliopo ambao serikali inalifanyia kazi pendekezo la kupitia kanuni na miongozo ya uchapaji viboko, si vibaya ikaweka washauri nasaha shuleni watakaokuwa wakisikiliza malalamiko ya wanafunzi.

# HABARI PICHA




Wabunge wakishindwa kujizuia kulia baada ya kuona jeneza lililobeba mwili wa Hayati Dk. John Magufuli mjini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Ndege za kijeshi zikipita juu ikiwa ni ishara ya kutoa heshima kwa aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli. **MPIGAPICHA WETU**



Mkazi wa Dodoma akitandika khanga yake ili gari lililobeba mwili wa Dk. John Magufuli liikanyage ikiwa ni kutoa heshima kwake. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Gari lililobeba mwili wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, likipita kuelekea Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma kwa ajili ya kuagwa kitaifa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Waombolezaji jijini Dodoma wakiwa nje ya Uwanja wa Jamhuri wakifuatilia matangazo ya moja kwa moja ya tukio la kuuaga mwili wa Hayati Rais Dk. John Magufuli. PICHA: RENATHA MSUNGU



Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Geita, Rose Busiga, akiangua kilio wakati jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli, ulipofikishwa jana, Bungeni kuagwa na wabunge hao. **MPIGAPICHA WETU**




# SALAMU ZA RAMBI RAMBI KUTOKA YAPI MERKEZI

Bodi ya Wakurugenzi, Uongozi na Wafanyakazi wote wa kampuni ya ujenzi wa reli ya SGR Tanzania, Yapı Merkezi tumepokea kwa mshtuko taarifa za kifo cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Pombe Magufuli.

Tunatoa salamu za pole kwa Rais Mama Samia Suluhu, Mama Janeth Magufuli, familia, ndugu na Watanzania wote. Tunaungana nanyi katika kuomboleza msiba huu mkubwa.

PUMZIKA KWA AMANI MCHAPAKAZI
DK. JOHN POMBE MAGUFULI
1959 - 2021

yapı merkezi

HABARI KITAIFA

## Wananchi waitwa vita kutokomeza bidhaa hafifu

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limewataka wananchi kushiriki katika 'vita' ya kutokomeza bidhaa hafifu hapa nchini ikiwa sehemu ya mchango wao wa kumuenzi aliyekuwa Rais wa Tanzania, John Magufuli katika ujenzi wa Tanzania ya Viwanda.

Wito huo ulitolewa kwa nyakati tofauti na maofisa wa TBS wiki iliyopita wakati wa kuhitimisha kampeni ya kutoa elimu kwa umma katika wilaya ya Musoma, Chato na Karagwe kuhusu umuhimu wa kununua bidhaa zilizothibitishwa na shirika hilo sambamba na kuwahamasisha wafanyabiashara kusajili maduka ya chakula na vipodozi.

Kampeni hiyo ya elimu kwa umma imefanyika katika maeneo mbalimbali yakiwamo ya shule za msingi na sekondari, masoko, stendi, minadani na maeneo mengine ya wazi ambapo wananchi walijitokeza kupata elimu na ufahamu wa masuala mbalimbali yahusuyo ubora wa bidhaa.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Musoma Mjini, Fidelica Gabriel Myovella, aliipongeza TBS kwa kutoa elimu kwa wananchi katika ngazi ya wilaya kwani itaongeza ufahamu na kuhakikisha suala la uuzaji wa bidhaa hafifu sokoni linapungua kama sio kwisha kabisa.

Ofisa Masoko, Deborah Haule aliwakumbusha wananchi kuwa vita ya bidhaa hafifu sio ya TBS pekee bali ni ya Taifa kwa ujumla.

"Kampeni hii imeweza kuwafikia wananchi 14,517 kati yao wanafunzi wa shule za msingi na sekondari 12,204 na wananchi 2,313," alisema Haule.

Haule aliwafafanulia wanafunzi pamoja na walimu umuhimu wa viwango katika maisha yao ya kila siku vile vile kuwafahamisha fursa ya huduma bure kwa wajasiriamali wadogo.

Hata hivyo, aliwaasa wawe mabalozi wazuri wa kuhamasisha ubora katika jamii wanazoishi.

Vilevile aliwasisitiza wananchi kuendelea kutoa taarifa pale wanapokutana na bidhaa zilizokwisha muda wake au wanapotilia shaka bidhaa yoyote katika soko na wafanyabiashara kufuatilia taratibu sahihi za usajili wa bidhaa au majengo kupitia mawasiliano waliyopewa.

Diwani wa Kata ya Bugene wilayani Karagwe, Mugisha Mathias, aliipongeza TBS kwa elimu ambayo wanaitoa katika wilaya hiyo kwani kuna baadhi ya wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla hawakuwa na elimu ya ubora wa bidhaa kwa undani zaidi.

# Jokate amlilia JPM siku ya kuzaliwa kwake

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo, amesema kuwa Hayati Rais Dk. John Magufuli, aliweka uhai wake rehani kwa ajili ya Watanzania, licha ya kuumwa ugonjwa wa moyo bado aliwatumikia kwa nguvu zote.

Katika ukurasa wake wa Instagramu aliandika; "Jana (juzi), Machi 20, ilikuwa ni kumbukumbu yangu ya kuzaliwa, lakini imekuja wakati ambao taifa tuko kwenye majonzi makubwa ya kuondokewa na Jemedari wetu, Rais wa awamu ya tano Dk. John Pombe Joseph Magufuli."

"Hivyo, nilitumia muda kutafakari maisha na kifo cha Rais (Magufuli), wetu mpendwa. Hakika maisha na uhai ni upepo tu. Lakini isitukatishe tamaa kufanya mema kadri ya Mungu atakavyotujalia ili tuweze kuacha alama."

Jokate alisema hayati Dk. Magufuli aliliongoza taifa kwa kujitoa licha ya maradhi ya moyo ya muda mrefu.

"Magufuli uliongoza taifa letu kwa kujitoa licha ya maradhi ya moyo ya muda mrefu, ukaweka uhai wako rehani kwa ujasiri, uthubutu, ubunifu na upendo mkubwa wa dhati kwa wananchi na taifa letu tukufu la Tanzania," alisema Jokate.

"Kama sehemu ya vijana uliotuamini kwenye serikali yako, tutaendelea kuenzi yako yote mema kwa ajili ya taifa letu mama la Tanzania kwa vizazi vya sasa na vijavyo." Nitoe pole kwa Mama Janeth Magufuli, familia yote na Watanzania wote. Bwana alitoa Bwana alitwaa jina la Bwana lihimidiwe."

Jokate ni miongoni mwa vijana walioteuliwa na hayati Dk. Magufuli kuongoza Wilaya ya Kisarawe.



Wapita njia wakiangalia nyumba ambayo ipo hatarini kubomoka kutokana na kutokuwa na kingo za kuzuia Mto Mbezi, katika eneo la Matosa, Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wamkumbuka Magufuli kwa visima virefu vya maji

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WAKAZI wa Kata ya Nyandekwa, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama Mji mkoani Shinyanga, wamesema watamkumbuka aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli, kwa kuwajengea visima virefu vya maji kwa kushirikiana na Jumuiya ya International Istaqama ya Oman.

Kata hiyo ilikuwa na visima vinne virefu vya maji vilivyojengwa tangu nchini ipate Uhuru wake mwaka 1961 ambavyo vilikuwa havitoshelezi mahitaji, lakini kwa sasa kunavisima virefu 100 ambavyo vinakidhi mahitaji ya wananchi wa kata hiyo.

Shedrack Daudi, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Nyandekwa, aliyabainisha hayo wakati akizungumza na gazeti hili na kusema amepokea msiba kwa masikitiko makubwa na kwamba watazidi kumkumbuka kwa kutatua kikwazo cha ukosefu wa majisafi na salama.

Alisema kabla ya ujenzi wa visima hivyo, walikuwa wanatumia maji ya kwenye visima vinne vilivyojengwa tangu Uhuru ambavyo havikutosheleza mahitaji na kusababisha baadhi ya wananchi kutumia maji ya kwenye mashamba ya mpunga ambayo sio safi na salama.

Aidha, Daudi alisema kwa sasa kata hiyo ina jumla ya visima virefu vya maji 100 na hivi karibuni kabla ya kifo cha Magufuli, wameahidiwa kujengewa visima vingine 20 vya maji, lengo likiwa kuendelea kutatua kikwazo cha ukosefu wa huduma ya majisafi na salama.

"Kifo cha aliyekuwa Rais kimetuumiza sana na alikuwa rais wa pekee aliyejali maisha ya kila Mtanzania bila ubaguzi wa kikabila wala dini...sisi tunashukuru kwa kuwapatia vibali watu wa Istiqama wa Oman na kutujengea visima vya maji," alisema Daudi.

Naye Josephina Juma, alisema hawakutegemea kama wangesongezewa huduma ya majisafi na salama kwa muda mfupi na kuwataka viongozi waliobaki kuyaishi yale aliyokuwa akiyafanya Magufuli katika kuendelea kutetea haki za wananchi wanyonge hasa wanaoishi pembezoni mwa miji.

Katibu Mtendaji wa Kamati Masjid Al-Wahaab, Ahmed Haroun, alisema amepokea kwa masikitiko makubwa msiba huo na kwamba walikuwa wakishirikiana pamoja katika kutatua kikwazo cha ukosefu wa huduma ya maji kwa wananchi wanaoishi pembezoni mwa miji.

# AfDB yaipiga jeki NIT bil. 4.7/- kupunguza ajali za barabarani

**Na Prosper Makene**

Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimeanzisha kituo cha kikanda cha umahiri katika usalama barabarani baada ya kupata msaada kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) wenye thamani ya dola za Marekani milioni 2.1 (zaidi ya Sh. bilioni 4.7 za Kitanzania).

Mkuu wa Chuo hicho, Mhandisi Prof. Zacharia Mganilwa, amesema: "Tunaishukuru sana Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa kutoa kiasi cha dola za Marekani milioni 2.1 ili kusaidia kuanzishwa kwa Kituo cha Umahiri, ambacho lengo lake kuu ni kufundisha wataalamu mahiri ambao watasaidia kupunguza ajali za barabarani."

Prof. Mganilwa aliongeza kuwa mkataba wao na Benki ya Maendeleo ya Afrika, na kwamba wamekubaliana kuanza kutoa kozi za ukaguzi ambazo zitawajengea uwezo wataalamu na hivyo kusaidia kupunguza ajali za barabarani.

Alisema Kituo cha Umahili kitaanza kutoa kozi hizo kabla ya mwaka huu kuisha mara tu watakapopata ithibati kutoka shirika la kimataifa linaloshughulika na usalama wa barabarani (IRF).

Alisema kwa sasa hakuna taasisi yoyote nchini inayotoa kozi za ukaguzi wa usalama barabarani kwa ngazi ya kimataifa hivyo NIT itakuwa taasisi ya kwanza kutoa mafunzo hayo.

"Watanzania na kampuni za kizalendo sasa wataweza kusoma kozi hizi zenye viwango na ubora wa ya kimataifa. Hakutakuwa na hitaji tena la Watanzania na kampuni kwenda kusoma kozi hizi nje ya nchi," alisema.

Alisema kampuni nyingi za Kitanzania zimekuwa zikipata tabu sana kwenye zabuni nyingi pale matangazo yanapotaka na kuhitaji kampuni wafanyakazi wenye sifa zinazotambulika Kimataifa.

Aliongeza, "Tunataka kuona miradi yote ya ujenzi na matengenezo ya barabara nchini inayohitaji wataalam wenye sifa hizi inakuchukuliwa na wenyeji."

Prof. Mganilwa alisema moja ya sharti katika mkataba wao na Benki ya Maendeleo ya Afrika ni kuwa kituo hicho kitaweka mshauri elekezi wa Kimataifa na kuwa na wataalamu 10 ambao watapata mafunzo ya kozi ya wakufunzi ili kuweza kuanza kutoa kozi hizo za usalama barabarani.

"Kituo kitachukua wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT), Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) ambao watapata mafunzo ya kozi ya wakufunzi juu ya usalama barabarani," alisema.



Dereva bodaboda akiwa na abiria huku amemweka mtoto mdogo mbele bila kuvaa kofia ngumu, katika eneo la Kimara Matosa Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mzee aliyempa JPM jogoo asafiri kumuaga

**Na Elizabeth Zaya**

ALIYEWAHI kumzawadia jogoo aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, Shaweji Kimbwembwe, amesafiri kutoka Somanga, Kilwa kuja jijini Dar es Salaam kutoa heshima za mwisho.

Akizungumza katika viwanja hivyo vya Uhuru, Kimbwembwe alisema ana haki ya kufanya hivyo kwa kuwa Hayati Magufuli amewafanyia mambo makubwa.

"Somanga ilikuwa na matatizo mengi sana ikiwamo vituo vya afya, barabara, kwa hiyo alipokuja Dk. Magufuli nilijitokeza na akanipa nafasi nikamweleza. Mpaka hivi tunavyozungumza, Somanga ina kituo cha afya bora kuliko vilivyopo katika Wilaya yote ya Kilwa, barabara nazo zinapitika," alisema.

"Ndio maana hata alipokuja tena nikaona nimpe zawadi ya jogoo kwa sababu alikuwa anastahili kupewa vitu vizuri zaidi."

Akizungumzia namna alivyopokea taarifa za kifo, Kimbwembwe alisema alishtuka sana baada ya vijana kwenda kumgongea usiku.

"Nilikuwa nimelala, nikasikia vijana wanagongea wananiambia amka mzee, Magufuli amefariki, kwa kweli nilishtuka, ikabidi niende kwa jirani kwenda kuangalia tv, nilivyofika kule ndio nikakuta wanatangaza, kwa kweli niliumia sana," alisema Kimbwembwe.

Alisema anaamini kwamba kwa mambo ambayo hayati Dk. Magufuli amefanya kwa nchi yake, Mungu atamlipa hata huko aendako.

"Mimi naamini kabisa kwamba Hayati Dk. Magufuli lazima atalipwa na Mwenyezi Mungu hata huko aendako kwa mambo makubwa aliyoyafanya kwa nchi yake, kwa sababu hata maandiko matakatifu yanasema anayetenda mema atalipwa mema," alisema Kimbwembwe.

# Benki ya Malawi yaipa ACB bil. 17/-

**Na Christina Mwakangale**

BENKI ya Akiba ya Biashara (ACB) ya Tanzania imepokea kiasi cha Sh. bilioni 17 kutoka Benki ya Taifa ya Malawi (NBM), ikiwa ni mkakati wa kuiimarisha kimtaji.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa ACB, Juliana Swai, alisema kuwa ushirikiano wa benki hizo mbili unategemewa kuleta mabadiliko chanya katika tasnia ya kibenki.

Swai alisema pia muungano wa ACB na NBM, ni mkakati mahususi wenye lengo la kupanua wigo wa kibiashara kwa ajili ya kuleta maendeleo zaidi kwa Watanzania, kuunga mkono ajenda ya serikali ya kuhakikisha kuna huduma shirikishi za kifedha nchini.

"Uwezo mkubwa na uzoefu wa taasisi hizi mbili katika sekta ya fedha, Benki ya Akiba imeweza kuimarisha mtaji, pia benki yetu itatoa huduma mpya zilizoboreshwa kwa mfumo wa kidijitali," alisema Swai.

Alisema fedha zilizotolewa na NMB kutaimarisha mtaji na kukidhi vigezo vya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kuhusu masharti ya kiasi cha mtaji wa uendeshaji wa benki ya kibiashara nchini.

Kadhalika, Swai alisema mabadiliko yanategemewa kuongeza fursa zilizokuwa zikitolewa na benki ya Akiba, na kupokea mambo mapya.

"Nawakaribisha wateja wetu wote pamoja na Watanzania katika benki yenu kwa ajili ya kufaidika na fursa nyingi ambazo zitawasaidia kuboresha maisha yenu pamoja na biashara zenu," alisema Swai.

"Tunaamini kuwa tutaweza kuwahudumia wateja wetu kwa weledi zaidi kupitia utalaamu na uzoefu wa taasisi hizi mbili bobezi katika sekta ya fedha, tunatambua mahusiano mazuri ya undugu na ya kibiashara kati ya nchi hizi mbili."

Alisisitiza kuwa benki ya ACB, kuwahudumia Watanzania kwa kutoa huduma zinakazokidhi mahitaji ya soko.

**"Nawakaribisha wateja wetu wote pamoja na Watanzania katika benki yenu kwa ajili ya kufaidika na fursa nyingi ambazo zitawasaidia kuboresha maisha yenu pamoja na biashara zenu," alisema Swai.**



# JPM alitekeleza elimu nchini kwa staili kuziba ombwe kwa falsafa ya Nyerere


**Na Peter Orwa**

MCHAKATO wa wananchi kumuaga kiongozi mkuu wa nchi, Hayati Rais John Magufuli uko katika hatua ya tatu leo, ikiwa fursa kwa wananchi wake kuagwa leo na wakazi wa Zanzibar.

Sasa umma uko katika lugha na tafsiri ya kukumbuka mema yake. Elimu ni moja ya maeneo ambayo hayatosahaulika katika ngazi mbalimbali iliyogawanyika katika pande kuu za vyuoni na shule.


Lakini, ili kujua kwa kina alichofanya hayati Magufuli, ni sharti kufahamu amewekeza katika msingi upi? Hapo ndipo historia inasonga mbali tangu zama za Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, ambao ulimuumba kiongozi huyo kutoka umri mdogo shuleni.

Hilo linaendelea katika awamu tatu za uongozi zilizofuata, kila moja ikiwekeza katika ngazi yake, kulingana na uhalisia wa mahitaji ya wakati na kabla ya kuacha kijiti kwa Dk. Magufuli.



Rais Dk. Magufuli. **PICHA ZOTE: MTANDAO**






### AWAMU YA KWANZA

Mara tu ya kupata nafasi ya kuongoza Tanganyika changa, Mwalimu Nyerere alitoa kipaumbele kwa elimu, ikiwa ni sehemu ya mpango mfupi wa maendeleo uliogota mwaka 1964.

Ni mpango uliofuta elimu ya matabaka, kuwapo shule maalum za jamii za Kizungu walipata nafasi zaidi, Waasia wakifuatia na mwisho Waafrika.

Mwendelezo wa utekelezaji wake kabla na baada ya mwaka huo wa 1954, ndio jijini Dar es Salaam, kunashuhudiwa shule za matabaka kuwa za umma, mathalan ikijumuisha Kisutu, Zanaki, Tambaza, Azania na Kibasila, ambayo hadi 1967, ilitwa St. Xavier.

Sura kamili ya alichokifanya Mwalimu Nyerere, inazama zaidi katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Taifa ambayo ilisimamia ujenzi wa viwanda vya msingi, huku elimu ya msingi kusambazwa katika ngazi ya vijiji, kuwapa uelewa na ujuzi Watanzania kutunukia nchi yao.

Ni katika awamu hiyo Mwalimu Nyerere mwaka 1967 alitangaza Azimio la Arusha, ambalo liliendana na kuzaliwa Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea.

Hapo Mwalimu Nyerere, alijikita katika dhana ya kwamba elimu inayotokewa nchini kuakisi maisha ya nchini; isitolewe kumjenga mtendaji wa ofisini (white collar job); msomi huyo ajiandae kujitumia jamii yake, mathalani ofisa kilimo.

Aidha, kila ngazi ya elimu ilitakiwa kujitgemea kumwandaa mtu kutumikia kimaisha, mathalan kidato cha nne au darasa la saba na mhitimu asihisi amefeli, bali kapata elimu ya kujimudu kimaisha.

Mwaka 1972, serikali ikiwa inatekeleza awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo, mwaka 1974, ilipitishwa Azimio la Musoma, ambayo katika namna fulani ilikuwa mwendelezo wa Azimio la Arusha, ikiwa na maudhui 'Elimu kwa Wote."

Utekelezaji wake ulishuhusiwa kuanzishwa madarasa ya kujifunza kusoma na kuandika jioni kwa watu wazima. Huku kukiandaliwa walimu wa kujitolea na walioandaliwa chini ya mpango wa muda mfupi maarufu UPE (Universal Primary Educatiion).

Ingawa wapo waliowadhihaki kwa UPE kubatizwa 'Ualimu Pasipo Elimu' lakini ukweli wa zao hilo lilikuwa juu sana, Tanzania kufikia kuwapo wa juu katika nchi ilifanya vizuri katika elimu kimataifa.

Ndani ya azimio hilo, ndio mwaka 1974 kukaundwa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), kukifuatiwa na mtaala wake wa mwaka 1976 na mwaka uliofuata iliundwa Bodi ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu (NBAA) ambayo pia ikawa msimamzi wa mitihani yake.

Hata katika ngazi ya vyuo, huku mbali na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, pia Chuo cha Mandeleo ya Uongozi Mzumbe (IDM) na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), vilianzishwa mwaka 1965.

Sambamba na hapo, kukawapo mwendelezo wa vyuo mbalimbali vya kisekta kama ardhi, afya, elimu na ufundi kama vile Dar Tech (sasa DIT) ambacho kilikuwapo tangu zama za ukoloni, vingi vilianzishwa katika zama kati ya miaka ya 1960 na 1970.

### MAHITAJI YA SEKONDARI

Kuanzia mwaka 1975, nafasi za shule za sekondari zilizokuwa chache, zikaanza kupanuliwa katika nafasi binafsi, Jumuiya ya Wazazi Tanzania (TAPA) ilipoanzisha shule nyingi nchini.

Pia kabla ya hapo Jumuiya ya Waislamu Tanzania (BAKWATA), kabla ya hapo ilianzisha shule nyingi binafsi za sekondari katika mikoa kama ya Dar es Salaam, Tanga na Kilimanjaro.

Kwa ujumla wake, ilikuwa na nafasi ya kuhamasisha mipango ya elimu ya nchi, hali kadhalika Azimio la Musoma, ikiendana na hitaji la wengi watakao fursa za kuendelea na elimu ya sekodari.

Pia ni muda mfupi baada ya hapo kukapitishwa Mpango wa Muda Mrefu wa Miaka 20 nchini, uliobeba maudhui ya mipango miwili ya maendeleo iliyopita, sasa katika mtazamo wa kina hata katika elimu, ikiwamo kuanzishwa vyuo vikuu vya aina kadhaa, ikiwamo Huria (OUT)

INAENDELEA UK.12



# JPM alitekeleza elimu nchini kwa staili kuziba ombwe kwa falsafa ya Nyerere



Rais John Magufuli akikata utepe kuzindua ndege mpya mbili aina ya Bombadier za ATCL, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam mwezi Septemba 2016. **PICHA: MAKTABA**

**INATOKA UK.11**

na Chuo Kikuu cha Madini.

Katika kipindi cha ukingoni kabla ya Mwalimu Nyerere hajaondoka madarakani, ni wakati hasa kukianza hamasa ya kuanzishwa sekondari binafsi za kata nchini, kuziba ombwe la fursa chache za sekondari zilizokuwapo wakati huo.

### AWAMU YA PILI

Kuingia kwa serikali ya awamu ya pili, iliendeleza juhudi za kupanua fursa za shule za sekondari kitaifa, serikali ikinga mkono kwa kuwaazima walimu kutoka serikalini na hasa katika nafasi ya mkuu wa shule.

Pia kukashuhudiwa mabadiliko, maana siasa na sera za uchumi wa nchi, sasa zilihamia katika ukiritimba wa dola na kuhamia mtazamo huria. Ni wakati ambao Rais wa awamu hiyo, Ali Hassan Mwinyi, alichukua hatua kadhaa ndani ya sekta ya elimu, inayojumuisha katika elimu ya juu kukatekelezwa sehemu ya Mpango wa Elimu ya Juu, kwa kuanzishswa Chuo Kikuu Huria.

Pia chuo kikuu pekee cha Dar es Salaam (UDSM), kilifanyiwa upanuzi wakati huo mwaka 1993 kikiwa na wanafunzi wastani chini ya 3000, kikifanyiwa upanuzi uliolenga kufikisha wanafunzi 4,000. Baadaye kuliendelezwa na sasa kina idadi kubwa zaidi ya mara nne ya ile iliyolengwa zaidi ya miaka 25 iliyopita.

> **“Katika yote haitosahaulika, alianza nafasi yake ya uongozi kwa ujenzi wa hosteli ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.**

Vyuo vingi binafsi vikaanza kuibuka na wakati huo huo, Rais Mwinyi alifanya maboresho makubwa ya maslahi ya wahadhiri wa vyuo vya elimu ya juu, hali iliyoweza kuwadhibiti, ikizingatiwa wapo walikuwa wakiondoka kusaka ajira ughaibuni na nchi jirani walikohitajika.

Katika shule, kulishuhudiwa mabadiliko ya mitaala, somo la elimu ya siasa kuondolewa kutoka ana mabadiliko ya sera ya nchi, ikichukuliwa somo la uraia.

Vivyo hivyo, mwaka 1985 ada ilianzisha rasmi katika shule za sekondari, vyuo vikuu nako ndio ukaanza mkopo mwaka 1994.


### AWAMU YA TATU

Uongozi wa Rais Benjamin Mkapa, umebeba historia kuu katika kujikita katika mpango wa ujenzi wa shule za sekondari za kata, ambayo ilichukua kasi kubwa, hali iliyogongana na uhaba wa hitaji la miundombnu na walimu, kutokana na uhalisia wa bajeti kitaifa.

Lakini zama ambayo kasi na idadi ya wanafunzi wanaojiunga na sekondari iliongezeka maradufu.

### AWAMU YA NNE

Moja ya mambo ambayo anakumbukwa Rais Jakaya Kikwete kujikuta nayo sana pale alianza nafasi yake ya uongozi, mbali na miundombinu na hasa barabara na Mpango wa Maendeleo ya Afya (MMAM), ulioanza rasmi




miaka mitano baada ya kuingia madarakani, kikuu alichofungua nacho mlango ni elimu.

Akijibu swalia alihojiwa na mwandishi wa kimataifa Thshaka Tsali, pale alipompatia takwimu za maendeleo ya sekondari za kata, Rais Kikwete, alimjibu kwamba anajikita katika kuea na uidai ya kutosha, huku wanaendeleza ubora, kulingana na uwezo wa nchi.

Baada ya muda mfupi, kulishuhudiwa namna aliyekuwa Waziri Mkuu, Edward Lowassa, alizunguka nchi nzima kukimbizana kuhakikisha miradi ya ujenzi wa shule za sekondari zinakamilishwa na kulishuhudiwa mafanikio.

Tija ya kazi hiyo, ilijionyesha pale taswira ya ushindi ilijiweka bayana, wananfunzi wanane kutoka shule za kata, waikuwa kati ya 20 waliofanya vizuri kitaifa, huku Waziri Mkuu wa baadaye, Mizengo Pinda, maarufu ‘Mtoto wa Mkulima’ aliguswa mno na kufanya nao sherehe.

Ndani za zama za Rais Kikwete, aliamua kuacha alama katika elimu ya juu, kwa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, kinachoingia katika vyuo vikuu vikubwa zaidi Kusini mwa Janga la Sahara.

Pia katika awamu yake, Rais Kikwete alihamasisha vyuo vikuu binafsi vingi kujengwa, akiweka masharti ya kuwa na vitivo vya ualimu, ili kuwezesha upatikanaji wa walimu wa kukidhi mahitaji ya sekondari za kata zilizoko kila kona nchini na mafanikio makubwa yameshuhudiwa.

### ZAMA ZA JPM

Kuingia madarakani kwa hayati Dk. Magufuli, aliitekeleza mahitaji ya sekta ya elimu katika tafsiri kuu mbili. Mosi, alifanya uchambuzi katika ombwe ndani ya sekta ya elimu na kugundua mambo kadhaa, ikiwamo kilio cha ada na matatizo katika namna ya upatikanaji mikopo kwa elimu ya juu.

Utekelezaji wake, umebeba sura ya kina katika mantiki ya Mwalimu Nyerere kati ya mwaka 1964 na 1969, iliyolenga kujenga mazingira wananchi wote kupata haki yao ya msingi, ambayo katika mazingira ya sasa imetoa hali hiyo.

Ushuhuda huo ulijionyesha pale Rais Dk. Magufuli, alipoanzisha elimu bure hadi sekondari mwitikio ukawa mkubwa, umma mkubwa ukajitokeza kuandikisha watoto wao shuleni, hali iliyotoa ishara kuna kundi kubwa lilikwama kupeleka watoto shule kwa sababu ya umaskini.

Hatua baada ya taarifa rasmi ya kifo chake, sehemu mojawapo ya mwangwi wa vilio ulitoka kwa wananchi baadhi ya wakimtafsiri “mkombozi wa elimu kandoka.”

Katika Sera ya Elimu nchini ambayo andiko lake la mwisho lililotolewa safari ya mwisho miaka miwili an Kamishna wa Elimu nchini, inadumu kwa miaka saba ijayo, ina maudhui ya ‘Elimu ya Kujitegemea’ ambayo ilitolewa na Mwalimu Julius Nyerere, mwaka 1967. Ni tafsiri tosha kwamba, Mwalimu Nyerere, anaendeleza mikakati ya elimu katikia falfasa na mipango ya Mwalimu Nyerere.

Katika yote haitosahaulika, alianza nafasi yake ya uongozi kwa ujenzi wa hosteli ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

***Je, alifanye kazi ni ilikuwa mzizi wa itikadi yake?***

***Usikose kesho siasa na uongozi wake.***

# Mwanazuoni: Ameondoka mwalimu mzuri wa somo la 'Maslahi ya Taifa'

**Na Sabato Kasika**

WATANZANIA wako katika siku 21 za maombolezo ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli, aliyefariki dunia ya jioni Jumatano iliyopita, jijini Dar es Salaam.

Mwili wake bado unazungushwa kwenye baadhi ya mikoa kwa ajili kuwapa watu nafasi ya kutoa heshima za mwisho kwa mpendwa wao. Leo ni zamu ya Zanzibar, kwa tendo la kitaifa na Ijumaa ijayo atapumzishwa nyumbani kwao Chato, mkoani Geita.

Ni kifo kilichogusa viongozi mbalimbali wa ndani na nje la bara la Afrika waliofika nchini kutoa heshima zao za mwisho, kuonyesha jinsi walivyokuwa wakitambua mchango wake kwa nchi na bara hilo.

Wakati hayo yakijiri, watu wa kada mbalimbali wamekuwa wakiendelea kumzungumzia kiongozi huyo walivyomfahamu na maono aliokuwa nayo kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii.

Miongoni mwao ni mchambuzi wa siasa na pia Mhadhiri katika Chuo cha Diplomasia Tanzania, Abbas Mwalimu, anayesema, Rais Magufuli alidhihirisha kwa vitendo dhana nzima ya maslahi ya taifa kwa nchi na kwamba alikuwa mwalimu bora wa somo alilolita 'Maslahi ya Taifa.'

"Kwa nini ninasema Rais Magufuli alikuwa mwalimu mzuri wa somo la Maslahi ya Taifa? Ili kufahamu sababu ni vyema kwanza tukafahamu maana ya neno maslahi ya taifa japo kwa uchache," anasema Abbas.

Anaeleza imani yake kwamba, Dk. Magufuli alikuwa mwanafunzi bora wa mwanafalsafa na mwanazuoni wa kimataifa, Niccolo Machiavelli, aliyeandika vitabu vingi vinavyolenga maslahi ya taifa.

Msomi hiyo wa sayansi ya siasa na diplomasia, anarejea andiko mojawapo analosema lilipendwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, kikiwa na mwelekeo wa kupigania na kulinda maslahi ya taifa, katika sura yenye kutafsiri rasilimali za taifa ndiyo inabeba uhai wa dola.

"Rasilimali za taifa zipo nyingi, kuna zinazoonekana na zisizoonekana, kwa mfano bahari, mito, maziwa, milima, mabonde, mbuga, wanyama, ndege, samaki, misitu, mapori, madini, bandari na hata watu wenyewe," anasema Abbas.

Pia mhadhiri huyo anamsifu hayati Dk. Magufuli, kwa namna alivyojikita katika upatikanaji kodi ya umma, ikiwa jambo linalobeba muktadha mpana wa maslahi ya taifa kwa wakati huu.





Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi, alipotoa taarifa katika Tamasha la 14 la Jinsia, Septemba mwaka jana, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**



Rais Dk. John Magufuli. **PICHA: MAKTABA**

"Tukumbuke pia Baba wa Taifa, aliwahi kusisitiza kwa kusema kuwa taifa lisilolipa kodi ni taifa mfu, kwa sababu kodi ndiyo uhai wa dola na hufanya dola kuwa na nguvu za kiuchumi na ushawishi," anasema.

Mhadhiri huyo anasema, kutolipa kodi kunaweza kusababisha taifa kuanguka na kwamba na katika kutambua hilo, Rais Magufuli alikuwa na jitihada binafsi za kukutana na wafanyabiashara, aliyewasisitizia haja ya ulipaji kodi, ili kuiwezesha dola kuwa na uhai wake.

"Kwa hayo na mengine mengi ambayo ameyafanya kwa miaka mitano, utagundua kuwa Rais Magufuli alikuwa ni mwalimu mzuri wa somo la Maslahi ya Taifa," anasema.

Mkurugenzi wa Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi, ana maoni kwamba tangu miaka ya 2000 wao walikuwa na kampeni iitwayo rudisha rasilimali kwa wananchi, nchi zetu za Afrika siyo maskini, bali tatizo analitaja liko katika mgawanyo wa mali.

Lilian akiwa anaongoza asasi inayosimamia maslahi ya kijinsia, anasema taswira ya kampeni yao ilijikita katika eneo hilo na anakiri serikali iliwaunga mkono, huku Rais Dk. Magufuli alitamka wazi kuwa nchi za Afrika siyo maskini, ikiwamo Tanzania, siyo maskini.

"Ni kweli nchi siyo maskini, kwani alisimamia vizuri rasilimali zote vizuri na matokeo yalionekana, hivyo tutamkumbuka kwa hilo na pia alivyosimamia uwajibikaji sehemu za kazi," anasema Lilian.

> **"Pia, niongeze kusema kuwa, Rais Magufuli ametangulia mbele ya haki na sasa nafasi imechukuliwa na aliyekuwa makamu wake, Mama Samia Suluhu Hassan ambaye hatuna shaka utendaji wake.**

Mkuu huyo wa asasi ya TGNP, anafafanua kuwa hali iliyojiri katika ofisi za umma ni kwamba watu walipofika kupata huduma katika ofisi wanapokelewa vizuri, ikiwa sekta ya afya, kwenye huduma za afya, zahanati nyingi zikijengwa vijijini na kwamba huduma zinapatikana.

"Pia, niongeze kusema kuwa, Rais Magufuli ametangulia mbele ya haki na sasa nafasi imechukuliwa na aliyekuwa makamu wake, Mama Samia Suluhu Hassan ambaye hatuna shaka utendaji wake," anasema.

Anafafaua kuwa baadhi ya mambo aliyoamua Rais Magufuli, aliyafanya kwenye uongozi wake na alipata ushauri kutoka kwa Rais wa sasa Samia Suluhu Hassan na kwamba TGNP ina imani naye katika nafasi hiyo ya urais.

"Tunaamini kwamba, kile ambacho Rais Magufuli alikianzisha kwa lengo la kunyanyua maendeleo ya nchi hii, Samia Suluhu Hassan atakiendeleza, kwa kuwa uwezo huo anao, tumpe ushirikiano," anasema.

Anahitimisha mtazamo wake Liliana ansema, Samia alifanya kazi bega kwa bega na Hayati Rais Magufuli na kuonyesha uwezo mkubwa, kama ilivyo kwa wanawake wengine, akitoa mfano wa Anne Makinda aliyewahi kuwa Spika Bunge la Tanzania.



UCHAMBUZI

# Namna uhai wa mawasiliano ulivyoguswa kila kona nchini

**Na John Mapepele**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, alitangaza msiba mzito kwa Taifa baada ya kutangaza tukio la msiba wa kitaifa.

Ni mara moja, mitandao ya kijamii ilikuwa ya kwanza kutoa habari kuonyesha mshtuko mkubwa wa kifo cha Rais Dk. John Magufuli, huku zikionyesha picha zake za video zenye ujumbe wa enzi za uhai wake.

"Siku moja mtanikumbuka na mimi ninajua mtanikumbuka kwa mazuri siyo kwa mabaya kwa sababu 'nime-sacrifice' (nimejitolea) maisha yangu kwa ajili ya Watanzania maskini.

"Kwa hiyo, tusimame pamoja tusibaguane kwa vyama, tusibaguane kwa ajili ya dini zetu, tusibaguane hata kwa makabila yetu, sisi tuijenge Tanzania," ni miongoni mwa picha hiso nya video yenye ujumbe ambao ulikuwa umetawala kwa takribani kwenye kila mtandao wa kijamii.

Kama mwanahabari mambo makubwa mawili yalinijia kwa haraka; kwenye kichwa changu baada ya kuona mitandao ya kijamii ikisambaza kwa kasi ya ajabu tukio hili la kifo.

Mosi ni namna Serikali ya Awamu ya Tano iliyoongozwa na Dk. Magufuli hadi umauti wake, ilivyoleta mageuzi makubwa kwenye mawasiliano ya kidigitali, kiasi kwamba habari inasambaa kwa haraka hivyo.


Hapo kuna busara ya kukumbuka katika awamu ya pili, Rais Dk. Magufuli alianzisha wizara maalum ya Sekta ya Mawasiliano, inayoongozwa na Daktari Faustine Ndugulile.

Vilevile, atakumbukwa kwa kuendelea kuimarisha sekta ya habari na utangazaji, inayobeba huduma ya jamii nchini, ambayo ni ni haki ya msingi ya raia iliyoko katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Hapo inatamka haki ya kila mtu kutoa nje mawazo yake, kutafuta, kupokea na kutoa habari na dhana zote kupitia chombo chochote, bila ya kujali mipaka ya nchi,

Lingine linalotajwa, ni uhuru wa mawasiliano kutoingiliwa, ni hali yao kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio nchini na duniani, ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za jamii.

Aidha, kuna suala la kutoa na kupokea habari, huku Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika, zina matamko rasmi ambayo serikali chini ya Dk. Magufuli imeyaridhia.



Hayati John Magufuli, alipokuwa katika moja ya ziara za kikazi. **PICHA: MTANDAO**

> **"Kama kiongozi imara, ni muhimu kusimamia wajibu wake na Dk. Magufuli anakuwa mfano kwa watakaofuatia, katika wajibu huo.**

Jambo la pili ambalo kwangu ndilo kubwa zaidi, ni ujumbe mzito na mahusisi kwenye video hiyo ambao kwa namna ya kipekee kabisa, ulimtambulisha Hayati Rais Magufuli tofauti kabisa na marais wengi Afrika na duniani kote.

Kule kujitoa maisha yake, kuwapigania wananchi hasa wanyonge, lakini zaidi ni kuweka taifa lenye mshikamano pasipo kubaguana kiimani, kabila au rangi, akimtanguliza Mungu katika kila jambo.

Ipo mifano ni mingi kwenye eneo hilo, itoshe tu kusema sekta kama madini ambayo awali kampuni za kigeni zilitumia kujinufaisha kupitia mikataba isiyofaa, wananchi kutoambulia cha maana.

Kuna sura nyingine ya kuboreshwa kwa miundombinu kama reli, barabara, viwanja vya ndege, ununuzi wa ndege na maboti, elimu, afya, kupiga vita rushwa, uwajibika kwa watumishi wa serikali, vyote aliweza kusimamia katika uhai wake.

Watu wanapomlilia katika kipindi kilichopo kila kona, wana maana inayojitosheleza.

**UGHAIBUNI**

Binafsi nilibahatika kusafiri naye katika ziara za kikazi kwenye nchi ya Namibia na Zimbawe mwaka 2019, ambako Serikali na wananchi wa nchi hizo, siyo tu walimsifu sana kwa usimamizi wake makini na kuwapigania wananchi wake, hata vyombo vya habari vya nchi hizo viliripoti kwa kumbatiza kuwa "tingatinga na jabali la Afrika limetua."

Hapo walibeba maana ya kiongozi shupavu na mfano wa kuigwa kwa viongozi wa Afrika amezuru nchi kwao.

Ni katika ziara hiyo, kila tulipofika na kabla ya kuondoka katika nchi moja na nyingine, alikuwa akielekeza na kusema naomba mmoja wetu Mkristo na Muislamu aombee safari yetu, kabla ya kuanza na kumaliza safari.

Baada ya kuingia kwenye ndege, kipekee nakumbuka mpiga picha wa Rais, Muhidin Issa Michuzi, ndiye aliyeomba kwa niaba ya dini ya kiislamu, mara baada ya kutua Uwanja wa Julius Nyerere, baada ya ndege kutua nyumbani.

**RC DK. NCHIMBI**

Mwanasiasa na msomi wa historia na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, anasema taifa limepoteza kiongozi makini, mnyenyekevu na mcha Mungu, ambaye amekuwa akilikabidhi taifa kwa Muumba.

Itakumbukwa, Dk. Magufuli, alikuwa wa kipekee duniani baada ya kuzuka ugonjwa wa corona duniani, alipokataa kuwafungia wananchi na badala yake akaja na dhana ya kulikabidhi taifa mbele ya Mungu.

Hapo suala la kufunga na kuomba kukafanyika kupitia imani tofauti, wananchi wakiendelea kuchapa kazi, hali ambayo nchi nyingine nyingi duniani zilishindwa.

Ni hatua yenye mwendelezo wa sasa, akilipa shaka kukubali kwa haraka kupokea chanjo ya kinga dhidi ya ugonjwa corona ambao tumeshuhudia hata nchi mbalimbali zilizoendelea kuanza pia kukataa chanjo hizo kutokana na ukweli kuwa chanjo hizo hazisaidii chochote.

"Kufa tutakufa tu unaweza kufa kwa malaria, ukafa kwa kansa, ukafa kwa magonjwa mengine kwa sababu kufa kupo lakini kamwe tusimwache Mungu, huo ndio wito wangu tusimame na Mungu" ni maneno aliyoyatoa Hayati Rais Magufuli tarehe 19 Februari, mwaka huu, akiwa Ikulu akisisitiza kumtanguliza Mungu kwenye kila jambo.

**WANANCHI WALIA**

Martha Samtweve, Mwinjilisti na Mwalimu mstaafu kutoka Kijiji cha Kifanya Njombe, anataja jambo ambalo Hayati Magufuli ameliachia ni kumtanguliza Mungu katika kila jambo.

Mwalimu Samtweve, anasema ni kipindi muhimu kwa Taifa kuenzi mambo yote aliyoyafanya husuan kutanguliza uzalendo wa taifa lake na kuacha kujilimbilikizia mali kama alivyokuwa akifanya Baba wa Taifa mwalimu Julius Nyerere.

Mufti na Shekhe Mkuu wa Tanzania, Abubakari bin Zuberi, amesema Rais Magufuli aliwasaidia sana wanyonge, kinamama, wanafunzi na kikuu kilichopo sasa ni kukubaliana na uhalisia chini ya kivuli cha imani.

Anasema kama kiongozi imara, ni muhimu kusimamia wajibu wake na Dk. Magufuli anakuwa mfano kwa watakaofuatia, katika wajibu huo.

***Mwandishi wa Makala hii ni Mkuu wa Kitengo cha Habari; Wizara ya Habari anapatikana kwa namba ya simu: 0784 441180 au jmapepele1@gmail.***



# ‘JPM alikuwa shujaa wa imani’

**Na PeterMkwavila, DODOMA**

ASKOFU wa Kanisa la International Evangelism Church Mkoa wa Dodoma, Sylvester Thadey, amesema kuwa Rais John Magufuli alikuwa ni shujaa wa imani aliyejitahidi kutenda haki na kutekeleza miradi ambayo inayogusa maisha ya Watanzania kwa ajili ya maendeleo ya wote.

Aidha, amesema Rais Magufuli, alikuwa ni mtu mwenye kuthubutu na mzalendo wa kweli kwa ajili ya taifa lake la Tanzania na kuweza kurejesha heshima kwa viongozi wa umma wa dini na jamii kwa ujumla.

Rais John Magufuli alifariki dunia Machi 17, mwaka huu, katika Hospitali ya Mzena jijini Dar es Salaam alikokuwa akipatiwa matibabu ya moyo.

Askofu Thadey alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye ibada iliyofanyika juzi kanisani hapo.

Alisema kuwa katika kipindi alichokaa madarakani Dk. Magufuli alimpenda na kumtanguliza Mungu kwa kila jambo ambalo lilikuwa akilisema kwa ajili ya Watanzania na hii imesababisha Tanzania kuinua uchumi wake na kuwataka Watanzania kuwa na mshikamao miongoni mwao na kuyaenzi mazuri aliyoyafanya enzi ya uhai wake.

Thadey alisema kuwa kutokana na jitiaada zake aliinua Taifa la Tanzania kiuchumi na kuifanya kuwa nchi bora inayoweza kujitegemea kwa kutekeleza miradi kwa mali na fedha za ndani bila kutegemea zaidi wafadhili wa nje.

Alisema kuwa Dk. Magufuli pia alikuwa shujaa wa imani asiye na ubaguzi wa dini na kwamba hata nidhamu iliweza kurejeshwa kwa watumishi wa umma ikiwamo na heshima mpaka kwa viongozi wa dini na watu wa hali ya chini.

“Magufuli alikuwa ni mtu aliyekuwa na hofu ya Mungu kila mara alisisitiza Watanzania tumtangulize Mungu kwanza, kwa kuwa kitendo hicho kilikuwa ni kama chanzo cha maendeleo makubwa ambayo pia aliyoibua mali za nchi, kodi na fedha,” alisema.

Pia aliwaomba Watanzania kuendelea kumwenzi Rais Magufuli kwa yale yote aliyotuachia kwa vitendo ili viweze kukamilishwa kwa wakati.

Alisema kuwa Magufuli alikuwa mzalendo wa kweli na mambo mengi aliyofanya yameacha alama itakayodumu katika maisha na vizazi vya Watanzania, hivyo viongozi na Watanzania kwa ujumla tuenzi maono hayo ambayo yaliyoanzishwa yapate kuendelezwa yote.

Alisema Magufuli aliweza kuzungumza na kila Mtanzania na alileta moyo mpya wa matumaini kwa nchi hasa kwa watu maskini wa nchi yake.

# Askofu amkumbuka JPM ujenzi nyumba za ibada

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

ASKOFU Mstaafu wa Kanisa la Evangelisti Assemblies of God Tanzania (EAGT), Ipagala jijini Dodoma, Evance Chande, amesema kuwa atamkumbuka hayati Rais Dk. John Magufuli jinsi alivyokuwa akihamasisha waumini wa madhehebu ya dini kuchangia michango mbalimbali ya ujenzi wa nyumba za ibada bila kujali itikadi ya dhehebu.

Kiongozi huyo wa kiroho alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kanisani kwake baada ya kumalizika kwa ibada maalumu kwa ajili ya maombi kutokana na msiba mkubwa wa taifa kuondokewa na Rais John Magufuli.

Alisema kuwa, Rais alitujengea uhusiano mzuri kwa waumini wote bila kujali dhehebu gani la dini katika kuhakikisha kila mmoja anawajibu wa kuchangia masuala ya kiroho ikiwamo michango ya nyumba za ibada.

Aidha, pamoja na kuhamasisha na kuimarisha upendo huo kwa waumini wa kuchangia michango nyumba hizo za ibada, pia kwenye kipindi chake cha uongozi wa miaka mitano atakumbukwa kwa kuanzisha miradi mikubwa ya kimaendeleo ambayo itakayobadilisha uchumi wa nchi.

Chande alisema kuwa Rais Magufuli, pia atakumbukwa zaidi kwa uzalendo wake wa kuwapenda Watanzania wa hali ya chini kwa vitendo ambao walio wengi waliweza kutatuliwa kero zao ikiwamo kundi la mama lishe na machinga.

Alisema kwenye kipindi chake cha uongozi Magufuli alifungua milango kwa mama lishe na machinga ambao walikuwa wakibughudhiwa na kuporwa mali zao na kuwasababishiwa umaskini na kushindwa hata kulipa kodi kwa serikali.

Askofu huyo aliwaomba Watanzania kudumisha maombi kwenye nyumba za ibada ili yale yote yaliyoachwa na John Magufuli yaweze kufikia malengo yake kwa wakati. Alisema miradi ni mingi ambayo rais ameiacha bila kukamilika hivyo yote hiyo inahitaji kuiombea ili iweze kukamilika kwa wakati hii ni pamoja na hata wale wanaosimamia wasikatishwe tamaa.

Askofu Chande, pia aliwaomba Watanzania kumwamini mama Samia Suluhu Hassan ambaye ni Rais kwa hivi sasa katika utendaji wake, kwani katika kipindi chake alichokuwa na Dk. John Magufuli amefanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania wote.



Wakazi wa Dodoma wakiwa wamepanda juu ya mbao nje ya Uwanja wa Jamhuri ili waweze kuona shughuli za kuuaga mwili wa hayati Rais Dk. John Magufuli zilizofanyika kitaifa mkoani humo, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Machinga watengewa maeneo maalum

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

BAADA ya wafanyabiashara wa mbao jijini Dodoma kupewa notisi ya kuhama katika baadhi ya maeneo waliyokuwa wakifanyia biashara zao, uongozi wa jiji umewaandalia maeneo maalumu.

Akizungumza na gazeti hili Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru alisema wamewaandali maeneo mawili katika kata ya Kizota na Nzuguni pembeni ya soko kuu la Job Ndugai.

Mafuru alisema lengo la kufanya hivyo ni kuepusha usumbufu wanaoupata wafanyabiashara.

“Wauza mbao walishapewa notisi ya kuondoka sasa hawana maeneo maalumu, na ukiangalia maeneo mengi unaona mbao zimezagaa, hasa eneo la Jamhuri unakuta mbao kontena, mbao kontena,” alisema Mafuru.

“Nimewaelekeza maofisa biashara na mipango miji waandae maeneo hayo na tayari tumeshaanza kufyeka ili kuanza kutumika,” alisema.

Aidha, alisema baada ya miezi mitatu wafanyabiashara hao watakuwa na maeneo maalumu ya biashara, na kuwa hiyo ni baada ya uongozi wa jiji kufanya nao kikao.

Alisema wanalenga kuwa na jiji la Dodoma lililopangwa, linalojiendesha kiuchumi na wananchi wake wajiendeshe kiuchumi hivyo ili kufanikisha hilo ni lazima kila mfanyabiashara awe na anuani ya kudumu.

Naye mmoja wa wafanyabiashara hao, Vera Ngamale, alisema jiji watakapokamilisha miundombinu katika maeneo hayo wahakikishe wanawahamisha wauza mbao wote ili kuleta manufaa katika biashara hiyo.

Alisema kama jiji halitawaondoa wauza mbao wote kwenye maeneo yao ya sasa watakaopelekwa kwenye maeneo hayo maalumu hawataweza kuendesha biashara zao kwani watakosa wateja.

“Wote waondolewe mjini na wateja waelekezwe kuwa mbao zinapatikana sehemu fulani hapo tutakuwa na uwezo wa kulipa kodi zote zinazotakiwa,” alisema.

Naye Ruth Jones alisema kwenye maeneo wanayofanyia biashara walikuwa na wateja kwani wapo katikati ya mji lakini changamoto ilijitokeza baada ya wamiliki wa maeneo hayo kuwataka waondoke.

Hata hivyo, alisema wanafurahi kuandaliwa eneo la kudumu licha ya kuwa katika hatua za awali watakuwa na changamoto ya kuwapata wateja.



HABARI MBEYA

# Wafanya ibada maalumu kumwombea hayati JPM

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

BAADHI ya wananchi na viongozi wa serikali mkoani Mbeya wamejikuta wakibubujikwa na machozi huku wakigalagala chini wakati wa ibada maalum iliyoandaliwa kwa ajili ya kuliombea taifa kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais, Dk. John Magufuli kilichotokea Machi 17, mwaka huu.

Maombi hayo ambayo yaliandaliwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na kuwashirikisha wananchi, viongozi wa serikali, wa dini na wa mila yalifanyika mwishoni mwa wiki katika uwanja wa mpira wa Kumbukumbu ya Sokoine, jijini hapa.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, ndiye aliyekuwa wa kwanza kuangua kilio na kugalagala chini kiasi cha watoa huduma ya kwanza kufika na kumbeba ili kumwondoa uwanjani hapo kumpeleka sehemu walikokuwa wameketi viongozi wengine. Baada ya Ntinika kuondolewa na nyimbo za kuabudu zikiendelea kuimbwa, wananchi waliohudhuria maombi hayo waliangua kilio na kuanza kugalagala chini hali ambayo iliwapa wakati mgumu waliokuwa wanatoa msaada.

Akizungumza wakati wa ibada hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, aliwataka wananchi wa mkoa huo kuwa wastahimilivu wakati huu wa majonzi ya kitaifa.

Aliwataka wananchi hao wasinung'unike na kuumia kutokana na msiba huo kwa kuwa kifo cha Dk. Magufuli kimetokea kwa sababu ya mapenzi ya Mungu na kuwaomba wananchi kuendelea kuliombea taifa.

"Tuendelee kumwombea Rais wetu mpya, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, atuongoze vizuri katika kipindi hiki cha maombolezo pamoja na kulimalizia vizuri kuliongoza taifa katika kipindi cha miaka minne iliyobakia," alisema Chalamila.

Baadhi ya viongozi wa dini waliopata nafasi ya kuzungumza kwenye mkutano huo, waliwataka wananchi kuendelea kumuenzi marehemu Dk. Magufuli katika kila jambo kwa kumtegemea Mungu kama alivyokuwa anasisitiza.

Mjumbe wa Baraza la Waislam Mkoa wa Mbeya, Sheikh Ayoub Shupavu, aliwaomba wananchi kuendelea kumwombea Rais Mama Samia aendeleze maono aliyokuwa nayo marehemu Dk. Magufuli, ikiwamo utekelezaji wa miradi.

Aliwataka viongozi wengine wa serikali kuendelea kufuata maelekezo yote yatakayokuwa yanatolewa na rais kama walivyokuwa wanatekeleza maelekezo ya Dk. Magufuli.

"Tumwombee sana Rais wetu mpya aliyemaliza kuapa muda huu (jana), ili aepushiwe mbali na maadui wa ndani na nje ya nchi, walioko juu na chini ambao wanapanga mipango mibaya dhidi yake," alisema Sheikh Shupavu.

Kwa upande wake Askofu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Konde, Edward Mwaikali, alisema marehemu Magufuli alikuwa ni chaguo la Mungu.

Alisema marehemu Magufuli alishaweka wazi kuwa yeye anajitoa kama sadaka kwa wananchi wa Tanzania kwa kutetea rasilimali za taifa na kuwaomba viongozi waliobaki waendelee kutetea maono yake hayo.

Katika maombi hayo, baadhi ya wananchi wakiwamo wafanyabiashara wadogo maarufu kwa jina la machinga na mamalishe wa Jiji la Mbeya walionekana wamebeba mabango yenye jumbe mbalimbali za kumsifu marehemu Dk. Magufuli.



Baadhi ya wananchi wa Mkoa wa Mbeya wakiwa wamejumuika na viongozi wa serikali mkoani humo, kwenye maombi maalumu ya kuliombea Taifa kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, yaliyofanyika katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# ...Waomba jina la uwanja wa ndege liwe Magufuli

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

BAADHI ya wananchi mkoani Mbeya, wameiomba serikali kubadili jina la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA) na kuuita Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Magufuli kama sehemu ya Kumuenzi aliyekuwa Rais wa Tanzania Dk. John Magufuli aliyefariki Machi 17, mwaka huu.

Walitoa ombi hilo jana walipokuwa wanazungumza na Nipashe kuwa pamoja na kiongozi huyo kufanya maendeleo makubwa mkoani humo, hakuna mradi wowote mkubwa ambao umepewa jina lake.

Mmoja wa wananchi hao, Lauden Mwambona, alisema kabla ya Rais Magufuli kufariki alikuwa na mpango wa kuuboresha Uwanja wa Ndege wa Songwe kwa kuujengea miundombinu ya kisasa yakiwamo majengo ya baridi ili utumike kusafirisha matunda na mboga zinazozalishwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema Dk. Magufuli aliahidi kuuwekea uwanja huo taa za kuongozea ndege ili ufanye kazi usiku na mchana tofauti na sasa unatumika mchana pekee.

"Pamoja na maono yake kiongozi huyo, amefariki kabla hajayatimiza, lakini ametuachia imani kwamba uwanja huo pamoja na miundombinu mingine aliyoianzisha itaendelezwa, sasa ni vema viongozi wetu waone namna ya kumuenzi," alisema Mwambona.

Alisema mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini imekuwa ikizalisha matunda, mboga na maua ya aina mbalimbali na kwamba uwanja huo ukiwekewa miundombinu ambayo Dk. Magufuli alikuwa anawaza kuiweka, itasaidia kuwahamasisha wananchi kuongeza uzalishaji.

Alisema hivi karibuni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alipokuwa ziarani mkoani Njombe, alieleza mpango wa serikali kuukamilisha uwanja huo hali ambayo ilileta matumaini ya uwanja huo kukamilika.

Naye Sylvester Juma, alisema katika Mkoa wa Mbeya kuna taasisi moja pekee ambayo imepewa jina la Dk. Magufuli ambayo hata hivyo ni ndogo na haiweki kumbukumbu ya kiongozi huyo vizuri.

Aliitaja taasisi hiyo kuwa ni Shule ya Msingi ya Mchepuo wa Kiingereza ya Jiji la Mbeya, Dk. John Magufuli, iliyopo katika Kata ya Iyela jijini hapa ambayo ilifunguliwa rasmi mwaka jana.

"Huku kwetu tumejionea miradi mingi mikubwa, ametujengea meli kubwa tatu kwenye Ziwa Nyasa, ametujengea Uwanja wa Ndege na kuna hospitali nyingi zimejengwa na zilizokuwapo ameziboresha, sasa kuna kila sababu tukamuenzi," alisema Juma.

Alisema Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe ni eneo sahihi la kumuenzi Dk. Magufuli kwa kuwa jina la sasa haliutambulishi Mkoa wa Mbeya na badala yake unaonekana kama upo mkoa jirani wa Songwe.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, hivi karibuni alisema serikali inakusudia kutumia Sh. bilioni 18 kuuboresha uwanja wa SIA ikiwamo kuuwekea taa za kuongozea ndege na kuboresha njia ya kurukia.

## Wajasiriamali, machinga wamlilia mkombozi wao

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WAJASIRIAMALI na wafanyabiashara wadogo, maarufu 'Wamachinga' jijini Mbeya wamesema kifo cha aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli ni pigo kubwa kwao kwa vile hawana uhakika kama serikali itaendelea kuwajali kama ilivyokuwa utawala wa kiongozi huo.

Baadhi ya wajasiriamali hao waliyasema hayo jana wakati wakifuatilia tukio la kuagwa kwa mwili wa marehemu Dk. Magufuli kupitia kwenye televisheni, jijini hapa.

Modest Mwafongo, ambaye ni mchuuzi wa viatu jijini Mbeya alisema kuwa watamkumbuka Hayati Dk. Magufuli kwa kuanzisha utaratibu wa kuwatambua wafanyabiashara wadogo nchini kwa kuwapatia vitambulisho vya ujasiriamali. Alisema vitambulisho hivyo viliwasaidia wajasiriamali wote wakiwamo wamachinga kutosumbuliwa na mgambo wa Jiji pale wanapofanya biashara zao tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma.

"Tutamkumbuka Rais wetu Magufuli kwa kutuondelea shida ya kunyanyaswa na mgambo wa jiji ambao kwa miaka mingi walikuwa wakitupiga na kutunyang'anya bidhaa zetu, lakini yeye akatukomboa kwa kutupatia vitambulisho na kukomesha kabisa unyanyasaji ule, sasa hatuna uhakika kama serikali itaendelea na utaratibu huo baada ya kuwa Rais wetu amefariki dunia," alisema Mwafongo.

Naye Maria Mwakabaga ambaye anauza kofia alisema yeye ni miongoni mwa wajasiriamali ambao waliwahi kunufaika na vitambulisho vya rais kwa kuwa alikamatwa na mgambo wa jiji, lakini baadaye wakamwachia baada ya kuonyesha. Alisema yeye katika maisha yake alipenda kuuza kofia pana kwa sababu hata Rais Magufuli alikuwa anapenda kuzivaa na hivyo akawaomba viongozi wa serikali waliobaki kuendelea kutekeleza maagizo aliyowaachia ikiwamo kuwathamini machinga.



## Zanzibar yatangaza siku ya mapumziko kumuaga JPM

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imetangaza kuwa leo ni siku ya mapumziko ili kutoa nafasi kwa wananchi kuuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli.

Kwa mujibu wa taarifa ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Khalid Salum Mohammed, mwili huo utaagwa majira ya asubuhi katika Uwanja wa Amani Mjini Unguja.

Wakati serikali imetoa taarifa hiyo, Chama cha Waandishi wa Habari WanawakeTanzania (TAMWA) Zanzibar, kimewataka wazazi hasa wanawake kuchukua tahadhari kubwa watakapokwenda kuaga mwili ili warudi nyumbani mwao wakiwa salama.

TAMWA imetoa taarifa hiyo kutokana kuwapo kwa taarifa ya matukio ya kukanyagana kwa watu katika Uwanja wa Uhuru, jijini Dar es Salaam wakati wa kuaga mwili.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema zinapotokea vurugu kama hizo waathirika zaidi huwa wanawake na watoto na kuwataka wazazi na walezi kuchukua tahadhari.

"Kwa msingi huo tunawaomba wazazi sana kutokuchukua watoto katika ghafla hiyo ili kuwalinda na kukanyagwa pamoja na matatizo mengine ya kutokuwa na raha katika kipindi hicho," alisema Dk. Mzuri.

Aliwataka wanawake kuangalia kanuni za afya na kukumbuka kuwa dunia ikiwamo Tanzania bado inakabiliwa na maradhi ya kupumua.

"TAMWA Zanzibar inawatakia kila la kheri wananchi wote katika kuuaga mwili wa aliyekuwa Rais wetu mpendwa na tunamuomba Mungu aifanikishe salama shughuli hiyo ili hatimaye mwili huo uende ukalazwe kwa salama," alisema.

# CHAKUWAZA yasema Magufuli alikuwa shujaa

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama cha Kuwaendeleza Washairi Zanzibar (CHAKUWAZA), Mussa Makame Dere, ametoa salamu za pole kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Zanzibar, familia pamoja na wananchi wote kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais Dk. John Magufuli.

Alisema Watanzania wapo katika majonzi makubwa ya kumpoteza kiongozi shujaa, mchapakazi, mzalendo, na mpenda haki ambaye aliwaweka Watanzania kuwa pamoja katika kuiletea nchi maendeleo.

Aliyasema hayo katika hafla ya maadhimisho ya siku ya washairi duniani iliyofanyika katika ukumbi wa Shule ya Mbadala, Rahaleo mjini hapa.

Alisema siku hiyo ya maadhimisho ya kuendeleza washairi imefika katika kipindi ambacho taifa lipo katika majonzi makubwa ya kumpoteza kiongozi wao.

"Taifa limepoteza kiongozi shujaa, mchapakazi na mzalendo kwa nchi yake sina budi kufikisha salamu zangu za pole kwa serikali, familia na Watanzania wote Mungu awape nguvu na ujasiri katika kipindi hiki kigumu cha maombolezo," alisema. Katibu wa CHAKUWAZA, Said Suleiman Ali, alisema kutokana na kifo cha Rais Magufuli chama kimewaomba washairi wote kutunga mashairi ya maombolezo kwa kueleza mambo mbalimbali aliyoyafanya katika nchi.

Hata hivyo, aliwataka washairi wote kuimarisha umoja na kujitokeza kwa wingi katika hafla ya kuuaga mwili wa Hayati Magufuli.

Alisema wamedhamiria kuitangaza siku ya washairi na kutambulika kama siku nyingine duniani kwa kuandaa shughuli mbalimbali ikiwamo makongamano, ziara pamoja na matamasha ili washairi na watu wote kuifahamu siku hiyo.

Alisema mashairi yamekuwa na umuhimu mkubwa kwa jamii, yanaelimisha na baadhi kuburudisha na kwamba UNESCO wameitambulisha siku ya Machi 21 kila mwaka kuwa ni ya washairi duniani.



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ACT- Wazalendo, Juma Duni Haji, akitia saini katika kitabu cha maombolezo ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli katika ukumbi wa Shekhe Idrisa Abdulwakil Kikwajuni Zanzibar, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wabunge wastaafu wamkumbuka kwa uzalendo

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WABUNGE wastaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliowahi kufanya kazi na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli , wamesema taifa limepoteza shujaa aliyefanya kazi kwa kuweka mbele uzalendo wa kupenda taifa lake.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kikwajuni, Parmukhi Hoogan Sigh, alisema uwezo na ubunifu wa marehemu Dk. Magufuli ulianza kujionyesha alipokuwa Waziri wa Ujenzi na katika Bunge la Jamhuri ya Muungano alionyesha uwezo mkubwa katika kujibu maswali na hoja na kufafanua mambo mbalimbali yaliyotokana na wizara yake.

Alisema nyota yake ilizidi kung'ara alipochaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano na alikua na kaulimbiu ya 'Hapa kazi tu' huku akitekeleza na kusimamia miradi mikubwa ya miundombinu kwa ajili ya kuijenga Tanzania.

Hoogan alisema mikakati hiyo iliiwezesha Tanzania kuingia katika uchumi wa kati kutokana na juhudi zake za kupambana na ubadhirifu, kuziba mianya ya rushwa na vita dhidi ya ufisadi.

Naye aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Chwaka, Yahya Kassim Issa, aliwataka Watanzania kuendelea kumkumbuka kiongozi wao kwa mambo makubwa aliyoyafanya katika kipindi cha uhai wake na kuwa mfano wa kuigwa katika kuleta maendeleo.

Issa alisema aliingia bungeni pamoja na Dk. Magufuli ambaye alionyesha uwezo na haraka kuchaguliwa Naibu Waziri na baadaye kupanda ngazi hatua kwa hatua hadi kufikia kuwa Rais wa Tanzania.

Kwa upande wake aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Jang'ombe, Mohamed Rajab Soud, alisema anakumbuka uwezo wa Dk. Magufuli, ambaye wakati alipokuwa mbunge akifanya kazi katika kamati ya ujenzi na miundombinu.

Alisema alijibu hoja mbalimbali za wabunge waliochangia bajeti yake huku akionekana kukidhi kiu ya wabunge.

HABARI KITAIFA

# Samia aombwa kurejesha mchakato wa Katiba mpya

**Na Frank Kaundula, MOROGORO**

MTANDAO wa watetezi wa haki za binadamu Tanzania umeeleza kusikitishwa na kifo cha aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli.

Umeiomba serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuyaenzi mazuri aliyoyafanya kisheria hasa kwa kurejesha mchakato wa Katiba mpya ya wananchi.

Rai hiyo ilitolewa jana na mratibu wa mtandano wa watetezi wa haki za binadamu, Onesmo Olengurumwa, wakati akizungumza na waandishi wa habari, ambapo alieleza kuwa Hayati Dk. Magufuli alifanyakazi kubwa ya kuijenga nchi katika kipindi kifupi alichokuwa madarakani.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano imeshuhudiwa Rais akitumia nguvu kubwa katika ujenzi wa miradi mikubwa ya kimkakati sambamba na kulinda rasilimali za nchi zisipotee kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, na kwamba katika kuenzi kazi yake iliyotukuka ni muhimu kupatikana kwa katiba mpya.

"Kifo cha hayati Dk. Magufuli kimetusikitisha sana kwa sababu tunajiuliza ni kwa namna gani nchi yetu itaenda pasipo na uwapo wake, miradi mikubwa aliyoianzisha, ukali wake kurejesha nidhamu serikalini pia kusimamia rasilimali za nchi zisiibwe," alisema na kuongeza:

"Hapa ndipo linakuja wazo la kutaka kurejeshwa mchakato wa katiba mpya ili kulinda alichoanzisha kisheria bila hivyo tutajikuta tunarudi tulipotoka."

Alisema katika awamu ya uongozi kuna changamoto zake ambazo wakati mwingine zinapaswa kutumia busara katika kuzitatua, hivyo serikali ya sasa inapaswa kuboresha sekta ya haki za binaamu ili kurejesha matumaini kwa wananchi walio wengi.

Alisema pamoja na mambo mengine, sekta hiyo bado inakabiliwa na changamoto ya baadhi ya viongozi hasa vyombo vya dola kushindwa kusimamia haki za wanyonge, huku wengine wakijikuta wakibambikizi kesi.

"Katika eneo tunaona Rais wetu Mama Samia anatakiwa kuliangukia kwa jicho pana ni kwenye haki za binadamu, na hapa ana kazi kubwa sana ya kufanya kuhakikisha kunakuwa na usawa kwa sababu changamoto ni nyingi kiasi kwamba hata wananchi kukosa imani na vyombo vyetu vya dola kwa sababu ya kubambikiwa kesi," alisema Olengurumwa.

Agustino Ernest ni Kaimu Mkurugenzi wa kituo cha wasaidizi wa kisheria Morogoro, alisema pamoja na mambo mengine, alisema kituo hicho kitamkumbuka Hayati Magufuli kwa jitihada yake ya kuhakikisha inatungwa sheria inayowatambua wasaidizi wa kisheria.

Alisema awali wasaidizi hao walikuwa hawatambuliki kisheria, jambo lililokuwa likisababisha baadhi yao kushindwa kutekeleza wajibu wao ipasavyo kutokana na woga tofauti na ilivyo sasa ambapo imesaidia wananchi wengi kupata haki zao.




Rais wa Zambia, Edgar Lungu, akitoa heshima za mwisho kwenye jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli, jijini Dodoma jana. **MPIGAPICHA WETU**

# Maandalizi ya kumuaga JPM Zanzibar yakamilika

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAANDALIZI ya kuuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, katika Viwanja vya Amaan Mjini Unguja yamekamilika.

Mwili utawasili majira ya saa 1:45 asubuhi leo katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume Unguja.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Raisi, Dk. Khalid Salum Muhammed, alisema kuwa baada ya kuwasili mwili huo ambapo utapokelewa rasmi na viongozi wa serikali na baada ya hapo utapelekwa Uwanja wa Amaan kwa kutumia gari maalum kupitia barabara za Kiembesamaki, Kwa Mchina, Mwanakwerekwe hadi Amaan.

Waziri huyo aliwataka wananchi kufika kiwanjani hapo mapema saa 12:00 za asubuhi ili kutulia kiwanjani hapo kwa ajili ya kupokea mwili huo ambao utaanza kuagwa majira ya saa mbili asubuhi.

**ACT YAFIKA OFISI ZA CCM KUTOA MKONO WA POLE**

Chama cha ACT-Wazalendo kimesema kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni pigo kubwa katika taifa na kuwataka Watanzania wote kuwa wavumilivu kipindi chote cha msiba.

Kauli hiyo ilitolewa na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Juma Duni Haji, akiwa katika Ifisi Kuu ya CCM iliyoko Kisiwandui Zanzibar kwa ajili ya kutoa mkono wa pole kwa viongozi wa CCM.

Alisema kuondokewa na mwenyekiti na akiwa Rais ni jambo zito sana na kusema inahitajika uwapo wa subra miongoni mwa Watanzania na familia na wana CCM.

Alisema kuwa Rais John Magufuli, alikuwa Rais aliyesimama katika majukwaa na kusema wazi kuwa anaunga mkono na ataendeleza maridhiano ya kisiasa Zanzibar.

"Sasa ni wajibu wetu sisi tuliohai kuyaendeleza na kuyaenzi ili walioanzisha ambao washatangulia mbele ya haki tuwatendee haki," alisema Haji.

Duni alisema viongozi wa CCM jinsi walivyowapokea katika serikali ya umoja wa kitaifa Zanzibar, maridhiano yaliosisiwa na Maalim Seif pamoja na baadhi ya viongozi wa CCM yanaendelezwa na kutekelezwa kwa vitendo.

Alisema kuwa viongozi wa Chama Cha Mapinduzi alipofariki aliyekuwa Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo walifika ofisini kwao Vuga kutoa mkono wa pole.

"Kwa hali hiyo tunaona ni kiasi gani maridhiano yanaendelezwa na tumeambiana kuwa Wazanzibar na Watanzania kwa jumla sisi ni wamoja tuendeleze umoja wetu," alisema Duni.

Duni Haji alieleza kuwa Wazanzibar ni wamoja na hapana budi kushirikiana hasa katika matukio hayo ya misiba ambayo yameshawahi kutokea.

Hata hivyo alisema matukio kama hayo huwa sababu nyengine ya kuwaunganisha Wazanzibar na kuweka pembeni tofauti zao za kisiasa na huungana pamoja katika kujega taifa.

"Hakuna mtu aliyetegemea kama matukio hayo ya kifo yatatokea lakini ni kazi ya muumba haina makosa," alisema Duni.

Aidha, Duni alisema kuwa marais walioopo sasa wote ni wapya na wanategemea kuwa na siasa za umoja na ushirikiano kwa maslahi mapana ya taifa.

"Tunampongeza mama Samia kwa kuchukuwa dhamana kubwa na tunategemea kuwa na siasa za maridhiano katika ardhi ya Tanzania," alisema.

# Kundi la vijana lazua taharuki Kariakoo

**Na Maulid Mmbaga**

KIKUNDI cha vijana wasiojulikana wamezua taharuki katika Soko la Kariakoo jijini Dar es Salaam na kusababisha maduka kufungwa, huku baadhi ya wafanyabiashara wakikimbia na kuacha bidhaa zao.

Tukio hilo lilitokea jana ambapo kikundi hicho cha watu kilikuwa kikipita sokoni humo, huku wakikimbia na wakiwataka wafanyabiashara kufunga biashara, wakidai kuwa kuna watu watawavamia kwa kuwa wamefungua biashara siku ya mapumziko ya kitaifa kwa ajili ya kuuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli.

Halima Hussein ambaye ni miongoni mwa wafanyabiashara katika eneo hilo, alisema kundi hilo la watu lilianza kukimbia huku likitisha watu kuwa watavamiwa jambo ambalo liliwatia hofu na baadhi yao wakalazimika kufunga kwa hofu.

"Baada ya kuona hali hiyo, watu walianza kukimbia huku wengine wakirudishia tu milango ya maduka yao bila kufunga vizuri na waliokuwa wamepanga bidhaa zao nje wengine walikimbia na kuziacha," alisema.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Jumanne Shauri, alisikitishwa na tukio hilo la kuzuiwa wafanyabiashara kuendelea na biashara zao eneo hilo kwa madai kuwa Machi 22 ni mapumziko kitaifa.

Pia alieleza kuwa maduka na wafanyabiashara wote waliopo katika maeneo ya jiji hilo kuendelea na biashara zao kama kawaida bila ya zuio lolote.

"Tudumishe amani na utulivu katika kipindi hiki ambacho taifa letu linaomboleza msiba wa aliyekuwa Rais wa Tanzania hayati John Magufuli," alisisitiza.

Kwa upande wake mkuu wa mkoa huo, Abubakar Kunenge, alisema hakuna agizo lolote lililotolewa na serikali kuhusu suala lililotokea, hivyo aliwataka wananchi kuwapuuza watu hao na waendelee na biashara zao.

"Hao waliofanya hayo ni wahuni na matapeli na tunaendelea kuchukua hatua za kisheria kwa waliohusika kulitekeleza hilo... pia nimewaagiza wafanyabiashara waendelee na biashara zao," alisema.

# Mgombea urais upinzani Congo afariki dunia

**Brazzaville, CONGO**

MGOMBEA wa urais wa upinzani nchini Congo - Brazzaville amefariki dunia akiugua Covid-19.

Guy Brice Parfait Kolelas, mmoja wa wagombea wakuu wa urais katika nchi hiyo, alifariki dunia Jumapili saa chache baada ya kukamilika kwa shughuli ya upigaji kura nchini humo.

Mkurugenzi wa kampeni yake, aliliambia Shirika la AFP kwamba, Kolelas aliaga dunia akiwa katika ndege ya matibabu iliyokuja Brazzaville kumchukua.

Mwanasiasa huyo mwenye umri wa miaka 61 alikuwa na virusi vya corona Ijumaa ilikuwa ya mwisho wa kufanya kampeni.

Uchaguzi wa Jumapili uliendeshwa kwa shwari ingawa, wapigakura wachache walijitokeza kushiriki uchaguzi huo kulingana na waangalizi.

Alikuwa mmoja wa wagombea sita wa upinzani waliokuwa wanawania kiti hicho dhidi ya Rais Sassou Nguesso.

Siku moja kabla ya uchaguzi picha ya video ilichapishwa ikimwonyesha Kolelas akiwa mnyonge akiwahimiza wapigakura kujitokeza kushiriki zoezi la upigaji kura.

Kolelas alikosa hafla yake ya mwisho ya kampeni Ijumaa baada ya kusema siku moja mapema kwamba anahofia alikuwa na malaria, Shirika la Habari la Associated Press liliripoti.

Alilazwa katika hospitali ya kibinafsi katika mji mkuu, Brazzaville na baadaye ilithibitishwa kuwa alikuwa na Covid-19.

Akiongea kwa Kifaransa kutoka kitandani mwake hospitalini, Kolelas alisema: "Ndugu zangu wapendwa, nina shida.

Ninapambana na kifo. Walakini, ninawauliza jitokezeni na kupiga kura kwa mabadiliko. Nisingepigania bure."

Mkuu wa timu ya serikali ya kupambana na Covid-19, Elira Dokekias, alisema kuwa hali ya Kolelas ilikuwa mbaya Jumamosi, Associated Press iliripoti.

Hali yake ilikuwa thabiti siku ya Jumapili kwa yeye kuhamishiwa kwenye kitengo cha corona katika hospitali ya chuo kikuu Brazzaville, na angepelekwa nje ya nchi kwa matibabu, Dk. Dokekias alinukuliwa.

Baada ya kupiga kura katika mji mkuu, Sassou Nguesso alimtakia afueni ya haraka, Kolelas.

Sasou Nguessou alimshinda Kolelas katika uchaguzi uliopita wa mwaka wa 2016, akipata asilimia 60 ya kura ikilinganishwa na 15% za mpinzani wake.

Kampuni inayofuatilia matumizi ya mitandao NetBlocks, iliripoti kwamba huduma za intaneti zilizimwa Jumapili kabla ya upigaji kura.

Chama kikubwa cha upinzani the Pan-African Union for Social Democracy (UPADS), kilisusia uchaguzi huo kikisema kinahofia kura hiyo italigawanya taifa.

Sassou Nguesso amekuwa madarakani tangu 1979, isipokuwa kipindi cha miaka mitano baada ya kushindwa uchaguzi mwaka 1992.

***BBC***



Majengo yakiwa yamezama kwenye maji kufuatia mafuriko eneo la Londonderry nje kidogo ya Magharibi mwa Sydney, nchini Australia, jana na kusababisha maelfu ya wakazi kuondolewa eneo hilo. **PICHA: AP**

# Maofisa wadaiwa kumuua mwandamanaji

**Mandalay, MYANMAR**

VIKOSI vya usalama vya Myanmar, vimemuua kwa kumpiga risasi mwandamanaji mmoja, wakati serikali ya Australia ikithibitisha kuwasaidia raia wake wawili waliokuwa kizuizini kujaribu kuondoka nchini humo.

Watu wawili walijeruhiwa wakati wa makabiliano ya vikosi vya usalama na waandamanaji.

Mamia ya madaktari na wauguzi waliandamana mwishoni mwa wiki katikati mwa Mandalay, mji wa pili kwa ukubwa Myanmar.

Takribani watu 250 waliuawa tangu kutokea mapinduzi Februari Mosi, mwaka huu na zaidi ya watu 2,300 wanashikiliwa.

Myanmar ilitumbukia katika mgogoro tangu wanajeshi walipomwondoa madarakani kiongozi wa kiraia Aung San Suu Kyi, mwezi uliopita, hatua ambayo ilichochea maandamano ya nchi nzima ya kudai demokrasia.

Mawaziri wa mambo ya kigeni wa Umoja wa Ulaya walitarajiwa kuwawekea vikwazo maofisa 11 wa kijeshi katika mkutano uliofanyika jana.

***DW***

**Myanmar ilitumbukia katika mgogoro tangu wanajeshi walipomwondoa madarakani kiongozi wa kiraia Aung San Suu Kyi, mwezi uliopita, hatua ambayo ilichochea maandamano ya nchi nzima ya kudai demokrasia.**

# UNESCO yaadhimisha siku ya ushairi

**New York, MAREKANI**

SIKU ya Ushairi Duniani, inayoadhimishwa kila Machi 21 kila mwaka na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), linakumbusha kwamba ushairi unaheshimika katika tamaduni zote.

Pia UNESCO inautaja ushairi ni moja wapo ya aina ya utajiri na zaidi ya utamaduni, unaojieleza kwa lugha na utambulisho. Maadhimisho hayo yanalenga kuhamasisha usomaji, uandishi na ufundishaji wa mashairi kwa kukuza mazungumzo ya kitamaduni na dansi, sanaa ya maigizo na uchoraji.

Moja ya malengo makuu ya siku hiyo ni kusaidia utofauti wa lugha kupitia ughani wa mashairi na kuzipatia lugha zilizo hatarini, uwezekano wa kusikika katika jamii zao.

Kwa mujibu wa UNESCO, ushairi ni mshirika mkuu wa uelewa kati ya watu na watu, kichocheo cha amani na mazungumzo. Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO, Audrey Azoulay, alisema kuwa mashairi yana uwezo wa kukumbusha kila mtu juu ya mnepo wa roho ya mwanadamu.

Mwaka mmoja uliopita, UN News iliwataka washairi, waandishi na wapenzi wa mashairi ulimwenguni kote kusimulia katika aya jinsi shida ya Covid-19 ilivyoathiri.

Siku ya Ushairi Duniani iliundwa mwaka 1999 wakati wa kikao cha 30 cha UNESCO, mjini Paris, nchini Ufaransa.

***UN***

# SUAREZ
## AFIKISHA MABAO 500




**MADRID, Hispania**

LUIS Suarez amefikisha mabao 500 kwenye maisha yake ya soka kwa klabu na timu ya taifa baada ya kuifungia Atletico Madrid kwenye ushindi wa 1-0 dhidi ya Deportivo Alaves, Jumapili.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Uruguay aliitumia vizuri pasi ya winga wa kulia Kieran Trippier na kufunga dakika ya 54 pale katika dimba la Wanda Metropolitano.

Alaves walikuwa na nafasi ya kusawazisha bao hilo, lakini golikipa wa Atletico Madrid, Jan Oblak aliokoa vizuri penalti ya Joselu.

Tangu alipoanza kucheza soka la kulipwa akiwa na Nacional timu ya nyumbani kwake na kufunga mabao 12, Suarez akazichezea klabu nyingine tano barani Ulaya.

Alifunga mabao 15 akicheza pale Groningen, 111 akiwa Ajax, 82 kwa Liverpool, 198 akicheza Barcelona, na sasa 19 akiwa Atletico.

Huku pia akiwa amefunga mabao 63 kwa timu ya Taifa ya Uruguay, na sasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, amefikisha mabao 500 aliyofunga kwa kipindi cha maisha yake ya soka.

Suarez pia ameshinda taji la Ligi Kuu Uruguay, Uholanzi na Hispania pamoja na Ligi ya Mabingwa na Copa America.

## SOLSKJAER ATAJA SABABU MAN UNITED KUTOLEWA FA

**LONDON, England**

OLE Gunnar Solskjaer amesema Manchester United haikuwa na namna yoyote ya kuweza kushinda kwenye mchezo wao wa robo fainali ya Kombe la FA dhidi ya Leicester City, kwani wachezaji wake walikuwa wamechoka.

Man United ilikubali kipigo cha mabao 3-1 kwenye mchezo huo wa juzi Jumapili na hivyo kuaga mashindano hayo hatua ya robo fainali.

Man United imetolewa kwenye FA ikiwa ni siku tatu baada ya kutoka kushinda 1-0 kwenye mchezo wa Ligi ya Europa dhidi ya AC Milan pale kwenye dimba la San Siro.

Mabao ya Leicester City yalifungwa na Kelechi Iheanacho dakika ya 24 na 78 na Youri Tielemans dakika ya 52, huku lile la Man United likifungwa na Mason Greenwood dakika ya 38.

Solksajer amesema wachezaji hawakuwa na maajabu kwenye mchezo huo kwa kuwa ni muda mfupi walikuwa wametoka kucheza na wamesafiri muda mrefu, jambo ambalo limewafanya wawe na uchovu.

Kocha huyo amesema hali inaeleweka kwa wachezaji namna walivyo pamoja na kushindwa kushinda hapo kwenye Uwanja wa King Power kwa kuwa wanacheza mechi moja kila baada ya siku tatu.

"Hatukuwa na chaguo na inaeleweka kwamba, kila baada ya siku tatu wachezaji wanacheza na hilo ni jambo kubwa na kila mechi ina ushindani," alisema Solskajaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Tumekuwa tukitumia muda pia kwenye safari kwa kuwa tunahitaji kufanikiwa, ni lazima hili tulimudu kwenye maisha yetu ya soka."



## Alaba amalizana na Barcelona

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA imefikia makubaliano na wawakilishi wa beki wa Bayern Munich na timu ya Taifa ya Austria, David Alaba, mwenye umri wa miaka 28, ili kuipata saini yake katika dirisha lijalo la majira ya joto.

Alaba ni mmoja kati ya wachezaji ambao rais wa sasa wa Barca, Joan Laporta alitoa ahadi kwamba ikiwa wanachama wa timu hiyo watampa nafasi ya kuongoza timu hiyo atahakikisha anamsajili.

Mazungumzo kati ya wawakilishi wa Barca na beki huyo yalianza mapema mwezi huu na taarifa zimetoka kwamba pande zote mbili zimekubaliana kufanikisha dili hilo mwishoni mwa msimu.

Kwa mujibu wa Marca, Rais wa Barca na wakala wa Alaba, Pini Zahavi, walikutana kabla ya uchaguzi mkuu na kukubaliana kwamba akishinda uchaguzi mchezaji huyo atakamilisha uhamisho.

Mkataba wake unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu kule Bayern na mbali ya Barca wababe wengine barani Ulaya kama Chelsea na Manchester United wamekuwa wakiwania saini yake.

Msimu huu amecheza mechi 33 za michuano yote akiwa na Bayern Munich.

## HABARI MICHEZO

# MBAPPE AFUNGA BAO LA 100 LIGUE 1

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe amefikisha mabao 100 aliyoifungia Paris Saint-Germain kwenye Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1.

Mbappe alifunga mara mbili Jumapili kuiwezesha timu yake kupata ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya Lyon.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, ambaye alianza kucheza soka akiwa na Monaco, alianza kucheza kwenye Ligi Kuu msimu wa 2015-16 kabla ya kuwa nyota na kuiwezesha kubea taji msimu uliofuata.


Na baadaye akasajiliwa na PSG, na Mbappe amekuwa mchezaji muhimu zaidi kwa kikosi hicho.

Mbappe pia amefikisha mabao 20 kwenye ligi hiyo msimu huu akiongoza orodha ya wachezaji waliofunga mabao mengi na kuwania tuzo ya Kiatu cha Dhahabu mwishoni mwa msimu huu.

# CHELSEA YAJITOSA KWA DONNARUMMA

**MILAN, Italia**

CHELSEA bado ipo kwenye vita na Manchester United na Juventus katika harakati za kuiwania saini ya golikipa wa AC Milan na timu ya Taifa ya Italia, Gianluigi Donnarumma, katika dirisha lijalo ikiwa hatosaini mkataba mpya.




Kipa huyo mwenye umri wa miaka 22, mkataba wake unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu na kumekuwa na sintofahamu ikiwa ataongeza mkataba mpya au la kutokana na lundo la timu zinazohitaji huduma yake kwa ofa nono.

Mwishoni mwa msimu huu, Chelsea inafikiria kuachana na Kepa Arrizabalaga na haina uhakika wa kuwa na Eduardo Mendy mwenye ubora au usawa kiafya kwa muda wote, hivyo inachohitaji ni kufanikisha dili la Donnarumma ili akaongeze ushindani kwa Mendy na kulifanya eneo hilo liwe bora zaidi.

Donnarumma ni mmoja kati ya makipa waliofanya vizuri msimu huu akiiwezesha Milan kuwa moja kati ya timu zinazofanya vizuri kwenye Seria A ikishika nafasi ya pili.

Kipa huyo tangu msimu huu uanze hadi sasa amecheza mechi 37 za michuano yote na kuruhusu mabao 44, huku mechi kumi kati ya hizo akimaliza bila ya kuruhusu nyavu zake kutikiswa.



# SALAH
## HATOMKARIBIA TENA RAMOS - CARLOS

**MADRID, Hispania**

NYOTA wa zamani wa Real Madrid, Roberto Carlos amesema haoni kama mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah atamsogelea tena beki Sergio Ramos katika mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Real Madrid imepagwa na Liverpool katika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ambapo Ramos na Salah watakutana tena.

Wawili hao kwa mara ya mwisho walikutana katika fainali ya michuano hiyo msimu wa 2017/18, na Salah aliumizwa na Ramos dakika za mwanzo tu za mchezo.

Katika mchezo huo uliopigwa huko Kiev, Salah akiumia bega na kumlazimu kutolewa nje ya uwanja, ambapo pia ilimpa ugumu katika maandalizi ya Kombe la Dunia 2018.

Mashabiki wa Liverpool tangu wakati huo wamemshikilia kumuona Ramos kama adui namba moja.

"Salah hataenda karibu na Sergio," alisema Carlos kwa kutania wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya ratiba hiyo.

"Litakuwa tukio ambalo litazungumziwa sana," aliongeza Carlos.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI AWEKA REKODI MPYA BARCA, LALIGA

Ampiku Xavi, sasa ni mchezaji pekee aliyefikisha mechi 768 kwa miamba hao wa soka la Hispania huku...

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi ameweka rekodi mpya kwa Barcelona, baada ya kufikisha mechi yake ya 768 kwa miamba hao wa soka la Hispania.

Messi awali aliifikia rekodi ya mchezaji mwenzake wa zamani wa 'Blaugrana' hao, Xavi wakati alipocheza dhidi ya Huesca Jumatatu iliyopita, akifikisha mechi 767 kwa klabu hiyo aliyojiunga nayo kwa mara ya kwanza akiwa na umri wa miaka 12.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, na kiungo wa zamani, Xavi ni wachezaji pekee katika historia ya klabu hiyo kufikisha mechi 700 wa miamba hao wa 'Catalunya', huku Andres Iniesta akiwafuatia kwa kucheza mechi 674.

Messi tayari rekodi yake hiyo inambeba kwa kutwaa mataji 34 na kufunga jumla ya mabao 658 kwa Barca, na aliifikia rekodi hiyo kwa staili yake akifunga mara mbili na kutoa pasi moja wakati wakishinda 6-1 dhidi ya Real Cociedad, juzi Jumapili.

Pia amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao 20 au zaidi kwa misimu 13 mfululizo kwenye LaLiga.

Hadi sasa Messi amecheza mechi 511 kwenye LaLiga, huku akicheza mechi 149 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, 79 kwenye Copa del Rey (Kombe la Mfalme), 20 kwenye Supercopa de Espana, tano kwenye Klabu Bingwa Dunia na nne kwenye UEFA Super Cup.

Messi anaongoza katika orodha yawafungaji bora kwenye LaLiga akifikisha mabao 21 msimu huu na Barca wapo nafasi ya pili wakipitwa pointi nne na vinara Atletico Madrid, ambao waliifunga Deportivo Alaves bao 1-0, Jumapili mchana.

Barca imeshinda mechi zake nane za ugenini kwenye LaLiga, na kuwafanya kucheza mechi sita bila kuruhusu bao.

## KWA UFUPI

**LIVER HAIJUI KUHUSU WIJNALDUM**
LIVERPOOL haijui chochote kuhusu kusaini mkataba wa awali kati ya Barcelona na kiungo wake, Georginio Wijnaldum, mwenye umri wa miaka 30. ***(Liverpool Echo)***

**ARTETA ANOGEWA NA ODEGAARD**
KOCHA Mikel Arteta amesema, Martin Odegaard ni kiongozi wa Arsenal akidokeza kwamba anataka kumsajili kwa mkataba wa kudumu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, ambaye anacheza hapo kwa mkopo kutoka Real Madrid. ***(Mirror)***

**PALACE KUMSAJILI DRAGUSIN**
KLABU ya Crystal Palace inaangalia uwezekano wa kumsajili mlinzi wa kati wa Juventus mwenye umri wa miaka 19, Radu Dragusin raia wa Romania. ***(Sun)***

**JUVENTUS WAMKOMALIA KEAN**
JUVENTUS ipo tayari kuwapa ofa Everton ya wachezaji wengine pamoja na fedha ili wamuachie mshambuliaji, Moise Kean mwenye umri wa miaka 21 kurudi klabuni hapo. ***(Tutto Juve via Teamtalk)***

**RUDIGER NA HATIMA YAKE**
MLINZI wa Ujerumani, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 28, atasubiri baada ya michuano ya Ulaya kabla ya kuamua hatima yake na Chelsea, ambako ana mkataba hadi Juni 2022. ***(Sun)***

**MORRISON KUTUA SHEFFIELD**
KIUNGO wa zamani wa Manchester United, Ravel Morrison mwenye umri wa miaka 28, anataka kusajiliwa na Sheffield Wednesday akiwa mchezaji huru. ***(Sheffield Star)***

**MUSSO AZIKATAA INTER, MILAN**
GOLIKIPA wa Udinese, Juan Musso, mwenye umri wa miaka 26 raia wa Argentina, amekataa ofa kutoka Inter Milan na AC Milan ili kujiunga na AS Roma. ***(Todofichajes)***

**SHVED AWANIWA UBELGIJI**
KLABU ya Mechelen ya nchini Ubelgiji inataka kumsajili kwa mkataba wa kudumu winga wa Celtic, Marjan Shved mwenye umri wa miaka 23, anayecheza hapo kwa mkopo. ***(Sportarena)***

**HANSI HATAINOA UJERUMANI**
OFISA Mtendaji wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge, amekanusha uwezekano wowote wa Hansi Flick kuchukua mikoba ya Joachim Low kukinoa kikosi cha timu ya Taifa ya Ujerumani. ***(Welt)***

**KNILL APEWA OFA SHEFFIELD**
KOCHA msaidizi wa Sheffield United, Alan Knill, amepewa ofa ya kubakia klabuni hapo baada ya kuondoka kwa Chris Wilder. ***(Sheffield Star)***

**KOKCU ATAKIWA ENGLAND**
LEICESTER City na Leeds United zinamwania kiungo wa Feyenoord, Orkun Kokcu mwenye umri wa miaka 20, ambaye anahusishwa na Arsenal na Sevilla. ***(La Razon, via Leicester Mercury)***

**BIELSA AWINDA STRAIKA**
KOCHA wa Leeds United, Marcelo Bielsa, amekanusha madai kwamba, anahitaji kuongeza mshambuliaji kwenye kikosi chake. ***(Mirror)***

# SIMBA YATOA SIRI MAFANIKIO LIGI MABINGWA AFRIKA 2021

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba umesema siri kubwa ya kupata mafanikio yanayoendelea katika timu yao ni uwekezaji ambao umefanywa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya klabu hiyo, Mohamed "Mo" Dewji, ikiwamo usajili wa kuimarisha kikosi chao kwa wachezaji wa kigeni.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema mafanikio ya timu yao kwa sasa ni uwekezaji uliofanywa husus an kwa kufanya usajili mzuri kwa kulenga michuano ya kimataifa.

Alisema haijawahi kutokea kwa timu kutoka Tanzania kucheza mechi zake nane kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kufungwa bao moja tu, lakini hilo msimu huu wamelifanya kwa kufungwa bao 1-0 katika michuano hiyo kwenye hatua za mwanzoni dhidi ya FC Platinum ya Zimbabwe kabla ya kufurumusha nje timu hiyo kwa jumla ya mabao 5-1 baada ya ushindi wa 4-0 Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye mchezo wa marudiano.

"Ni mechi hiyo ndio walitufunga nyumbani kwao, mfungaji wa bao hilo ni mchezaji wa Simba kwa sasa (Perfect Chikwende), baada ya hapo hakuna timu ambayo imeweza kutufunga hadi kufika hatua hii, nina imani na kikosi cha timu hii tutafika robo fainali na rekodi nzuri," alisema Barbara.

Alisema haijawahi kutokea kwa timu kufanya vizuri katika michuano hiyo, na Simba inakuwa timu ya kwanza ambayo yote hayo yametokea baada ya uwekezaji mzuri wa Mo Dewji.

"Licha ya kuwekeza katika timu, lakini pia umoja na mshikamano wetu ni silaha kubwa ambayo imetufikisha hapa, tuwahakikishie mashabiki kwamba malengo yetu ni kucheza robo fainali ya michuano hiyo," alisema Barbara.

Alisema wakati ligi ikisimama kupisha maandalizi ya timu za taifa kuwania kufuzu Afcon 2021, huku wachezaji wao wengi wakiungana na mataifa yao, waliobaki wanaendelea na mazoezi kwa ajili ya maandalizi ya mechi yao ijayo dhidi ya AS Vita ya DR Congo.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, alisema mechi mbili zilizobaki ni muhimu na anahitaji kuona wachezaji wake wakipambana kupata matokeo mazuri ikiwamo dhidi ya AS Vita ambayo watakuwa nyumbani katika Uwanja wa Mkapa, Dar es Salaam.

"Mechi zilizobakia ni ngumu sana, kwa sababu tunahitaji pointi moja ili kutinga robo fainali, si rahisi kwa kuwa mechi zote zinaushindani mkubwa kutokana na jinsi wapinzani wetu wawili wanahitaji ushindi ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kucheza hatua ya robo fainali," alisema Gomes.

Simba inaongoza Kundi A ikiwa na pointi 10 ikifuatiwa na Al Ahly yenye alama saba, AS Vita pointi nne na Al-Merrikh ikiburuza mkia kwa pointi yake moja.

MAISHA MAPYA...



Mshambuliaji wa zamani wa Simba Queens, Mwanahamisi Omar 'Gaucho' (kushoto), akiwa na wachezaji wenzake wa timu yake mpya, Chabab Atlas Khenifra (feminine) baada ya kuishuhudia ikiichapa OCK bao 1-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Morocco iliyopigwa juzi nchini humo. **PICHA: MTANDAO**

## Dodoma Jiji FC yaanzia gym

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Dodoma Jiji, imeanza mazoezi ya utimamu wa mwili 'gym' kwa ajili ya kujiandaa kwa Ligi Kuu Tanzania Bara, pamoja na michuano mingine baada ya kumalizika kwa siku 21 za maombolezo ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Moses Mpunga, amesema wachezaji wa timu hiyo wameingia gym juzi na wanaendelea na mazoezi ili mechi zitakapoanza wawe tayari wapo fiti.

"Tumeanza mazoezi ya utimamu kwa mwili, tunakiandaa kikosi chetu ili ligi ikianza wachezaji wawe fiti," alisema.

Mpunga pia alikuwa mmoja wa watu waliokwenda kutia saini kitabu cha maombolezo ya kifo cha Dk. Magufuli mjini Dodoma, akiiwakilisha klabu yake. Jana mwili wa Hayati Dk. Magufuli ulikuwa mjini Dodoma, baada ya kuwasili juzi jioni.

Kwa sasa michezo yote nchini Tanzania imesimama kupisha siku 21 zilizotangazwa maombolezo za kifo cha Dk. Magufuli, aliyefariki Machi 17 kwenye Hospitali ya Mzena jijini Dar es Salaam kwa matatizo ya moyo.

Dodoma Jiji inashika nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi 34 kwa mechi 24 ambazo imecheza mpaka sasa wakati huu Yanga ikiwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 50 ikifuatiwa na Simba yenye alama 46, lakini ikiwa na mechi tatu mkononi.

Dodoma Jiji itashuka dimbani tena Aprili 7, mwaka huu, ugenini katika Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga kuivaa Tanzania Prisons kwenye mechi ya Ligi Kuu.

Mchezo huo unatarajiwa kuwa mgumu kwa kila timu, kwani Prisons yenye pointi 31 katika nafasi ya nane, lakini ikiwa imeshuka dimbani mara 23, itahitaji ushindi ili kufikisha alama sawa na Dodoma Jij.

# Biashara United yataja sifa mrithi wa Baraza

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Biashara United imeanza mchakato kabambe wa kusaka kocha huku ikitangaza sifa anazopaswa kuwa nazo, baada ya aliyekuwa Kocha Mkuu, Mkenya Francis Baraza, kutimkia Kagera Sugar.

Kikao cha Kamati ya Utendaji wa klabu hiyo ikilichokaa juzi, Machi 21, kilimteua Marwa Chamari kuwa kocha msaidizi wa timu hiyo akishika kwa muda nafasi ya Baraza, huku mchakato wa kutafuta kocha ukiendelea.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya klabu hiyo, kupitia mtandao wake wa kijamii, awali Chambari alikuwa kocha msaidizi, hivyo kamati imeazimia kwa kauli moja kumpandisha kukaimu nafasi ya kocha mkuu hadi watakapompata mrithi wa mikoba ya Baraza.

Wakati hayo yakiendelea, klabu hiyo imetoa tangazo lake rasmi kwenye mtandao wake wa kijamii kusaka kocha, ikiwataka watu wote wenye sifa hizo kuandika barua rasmi kwa ajili ya kuomba nafasi hiyo.

Katika tangazo hilo, klabu hiyo, imebainisha vigezo kuwa anatakiwa kocha mwenye Leseni A ya ukocha kutoka Shirikisho la Soka Afrika (CAF) au zaidi, lakini awe na uzoefu wa miaka mitano na kuendelea wa kuzifundisha klabu za Ligi Kuu ya nchi yoyote kwa mafanikio.

Sifa nyingine ni kwamba kocha anayetakiwa ni yule ambaye pia ana uzoefu wa kuzifundisha timu za taifa kwa mafanikio kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati au Afrika nzima.

Klabu hiyo pia inataka kocha wao mpya awe anaweza kufundisha soka kwenye mazingira yoyote, na anayeweza kuandika vizuri lugha ya Kiswahili, Kingereza au vyote kwa pamoja kwa ufasaha.

Baraza ametimkia Kagera Sugar na kuiacha timu hiyo kwenye nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi 39 kwa mechi 23 ambazo imecheza mpaka sasa.

Michezo
Jumanne Machi 23, 2021
Nipashe



## MESSI AWEKA REKODI MPYA BARCA, LALIGA

HABARI UK 22

LA KUCHOMOA...




Mshambuliaji wa Arsenal, Alexandre Lacazette, akiifungia timu yake bao la kusawazisha kwa kichwa wakati ikitoka sare ya mabao 3-3 dhidi ya West Ham United, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa katika Uwanja wa London juzi. **PICHA: MTANDAO**

## STARS YAPANIA 3 ZA EQUATORIAL GUINEA

**Na Saada Akida**

WAKATI Kikosi cha timu ya Taifa ya Soka ya Tanzania `Taifa Stars`, kikitarajia kushuka dimbani keshokutwa nchini Equatorial Guinea kuwavaa wenyeji hao kwenye mechi ya kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2021, matarajio ya ushindi ni makubwa licha ya kukosa mechi moja ya kujipima nguvu, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Cliford Ndimbo, alisema kutokana na msiba mkubwa ulioikumba nchi kwa kumpoteza aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, wameshindwa kucheza mechi ya marudiano ya kirafiki dhidi ya Kenya (Harambee Stars), lakini kikosi hicho kinaendelea na mazoezi jijini Nairobi na wana matumaini makubwa ya kufanya vizuri dhidi ya Equatorial Guinea na baadaye watakaporejea nyumbani kuikaribisha Libya.

"Kocha Kim Poulsen alihitaji mechi mbili za kirafiki, tulicheza moja dhidi ya Kenya, tulitaka kurudiana ila haikuwezekana kwa sababu ya msiba mzito ulioikumba nchi yetu, kikosi kipo kambini Nairobi kikiendelea na maandalizi dhidi ya Equatorial Guinea," alisema Ndimbo.

Alisema maandalizi hayo yanaendelea vizuri na wanaimani ya kufanya vizuri katika michezo hiyo kulingana na programu ya mazoezi ya timu hiyo yanavyoendelea jijini Nairobi.

# SIMBA ITAFIA KWA MKAPA - AS VITA

### Ibenge asema anafahamu haifungi nyumbani lakini hakuna namna ushindi lazima, Gomes naye anena...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Simba ikieleza inahitaji kuhakikisha inapata alama moja tu katika mchezo ujao wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya AS Vita ya DR Congo ili kufuzu hatua ya robo fainali ya michuano hiyo, Kocha Mkuu wa Wakongomani hao, Florent Ibenge, amesema wanachotaka ni ushindi tu kwenye mechi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Aprili 3, mwaka huu.

Ibenge ameweka wazi kuwa timu yake ni lazima ishinde mechi zake mbili zilizobaki kwenye Kundi A, moja ikiwa dhidi ya Simba ili kupata nafasi ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo msimu huu.

Timu hizo zitakutana katika raundi ya tano ya michuano hiyo hatua ya makundi wakati huu Simba ikiongoza Kundi A ikiwa na pointi 10 ikifuatiwa na Al Ahly ya Misri yenye pointi saba huku AS Vita ikiwa na alama nne na Al-Merrikh ikiburuza mkia kwa pointi yake moja.

Ibenge amesema tayari amewaeleza wachezaji wake kuhakikisha wanashinda mechi mbili zilizobaki wakianza dhidi ya Simba, ambayo wataifuata katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, wakijua wazi kuwa timu hiyo haijapoteza mechi yoyote ikiwa uwanja wake wa nyumbani.

"Tunahitaji kushinda mechi zetu mbili zilizobaki dhidi ya Simba na Al-Merrikh ya Sudan ili kusonga mbele hatua ya robo fainali," Ibenge alisema.

"Matokeo ambayo tumeshayapata hayajawa mazuri kwetu, lakini huu si wakati wakuanza kulaumiana, tunachotakiwa kukifanya ni kuendelea kushinda mechi zetu zilizobaki."

Baada ya mechi hiyo, AS Vita itarudi nyumbani mjini Kinshasa kuikaribisha Al-Merrikh Aprili 9, mwaka huu, wakati siku hiyo Simba ikiwa ugenini nchini Misri kuivaa Al Ahly.

Kauli hiyo ya Ibenge, imekuja siku chache baada ya Kocha Mkuu wa Simba, Mfaransa Didier Gomes Da Rosa, kueleza malengo yao makuu na timu yake kwenye michuano hiyo ya CAF ni kuhakikisha wanatinga robo fainali.

"Kuipeleka timu hatua ya [robo fainali] inawezekana kabisa, shukrani kwa ushirikiano ninaoupata kutoka kwa viongozi, wasaidizi wangu na wachezaji ambao wanakiu kubwa ya mafanikio," Gomes alisema mwishoni mwa wiki.

"Kama utatazama, tunaongoza kundi letu na tumebakiza mechi mbili, moja tutacheza nyumbani dhidi ya AS Vita na nyingine ugenini dhidi ya Al Ahly, kama tutafanya vizuri ni wazi tutamaliza kileleni mwa msimamo wa kundi."

Simba haijapoteza mechi yoyote katika hatua ya makundi na pia haijaruhusu bao lolote, ikianza kwa kushinda ugenini bao 1-0 dhidi ya AS Vita kabla ya kurudi nyumbani na kuibuka na ushindi kama huo dhidi ya Al Ahly kisha ikasafiri kuifuata Al-Merrikh ya Sudan na kutoka sare tasa, kabla ya kuwakaribisha Wasudan hao katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na kuwachapa mabao 3-0.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002